COMMON SALVATION

W O K O V U W E T U

S O T E

NA

DAVID B. WARD

Chapishwa na:
United Pentecostal Church of Tanzania
SLP 1271
Moshi

ORODHA YA YALIYOMO

1. Wokovu Waelezwa Maana Yake..... 1
2. Fundisho la Toba..... 2
3. Uweza wa Nguvu za Jina la Yesu..... 7
4. Jina la Yesu katika Kanisa la kwanza..... 10
5. Wokovu katika Jina..... 14
6. Mathayo 28:19 - Kunukuliwa au kutiiwa?..... 19
7. Tutendeje?..... 21
8. Roho wa Ahadi..... 25
9. Fundisho la Ushahidi..... 31
10. Wokovu Mifano na Vivuli..... 36

WOKOVU WAELEZWA MAANA YAKE

Uchunguzi wa kina wa somo la wokovu hufunua mambo mengi. Kitabu kikubwa sana kingeweza kuandikwa pasipo kumaliza somo hili. Kwa hakika Biblia yenyewe imeandikwa kwa dhumuni hilo hasa; Kutuelekeza sisi kwa Mungu na kutuonyesha njia ya kuokolewa.

Wokovu kama somo ambalo ni lazima kujumuisha kutazama hali yetu ya upotovu na kutolewa kwa Mwokozi, pia mambo yanayoleta upatanisho, msamaha, ukombozi, kutambulishwa na Kristo, utii, ushindi juu ya dhambi, utakatifu na kuhesabiwa haki.

Mambo yote hayo yaliyotajwa hapo juu ni sehemu ya wokovu wetu. Neno la Mungu linajitosheleza kwa haya maneno. Hii si kusema kuwa mtu ni lazima aelewe kwa usahihi mambo yote haya ili yamtokee. Kuokoka kunakamilishwa kwa Ushirikiano wetu na tendo la neema ya Mungu.

Baadhi wangesema kuwa tungeweza kujifikiria tumeokoka baada ya kutimiza Uzao mpya. Wengine wangeshindana kuwa hatua za wokovu hutuchukua mbali zaidi ya hilo na kutupeleka kwenye utakaso na uzima wa milele. Mjadala huu ni suala halisi la maana ya lugha inayohusu maneno na jinsi yalivyokua, ambao hauwezi kutatua vya kutosha. Katika mchanganuo wa mwisho - tunachopaswa kufanya ni kumpendeza Mungu naye atashughulikia yaliyosalia.

Kitu kinachotokea mara nyingi ni kuwa yaliyo ya kadiri na kuupa jina kuwa ndiyo mpango wa wokovu. Wakati huo unaweza kuwa dhahiri kwa kutufanya tuingie katika Ufalme kwa hakika Mungu hutukusudia zaidi ya hilo. Hatari ya mtazamo huu wa kurahisisha ni kuwa wakati mwingine tunamtupa mtoto pamoja na maji ya kumwogesha tunapotaka kuamua ni lipi linalohitajika na ni lipi halihitajiki. Hii inaonekana katika madhehebu mengi ambapo mpango wa Mungu umepunguzwa na kubaki ukiri mtupu au kupokea wokovu kwa kujitwalia neema kidogo ya Mungu.

Huenda hatima ya wokovu wetu ilielezwa pale mwanzo kabisa wakati Bwana alitamka kusudi lake la kumfanya mtu kwa sura yake mwenyewe. Ahadi ya Mungu katika 1 Yohana 3:2 inaonekana kuonyesha jambo hili.

"Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhihirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhihirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo" (1Yohana 3:2).

Wote tunaweza kukubali kwamba tutakapoamka katika mfano wake tutakuwa tumeokoka pasipo shaka. Sisi sote tutakapofikia katika hali ile baada ya kuishi maisha tofauti kabisa na kuwa na vipimo tofauti kabisa vya Imani na neema ya Mungu, ni dhahiri kabisa kutokana na Neno la Mungu kuwa wote ni lazima tuwe tulianzia mahali pale pale. Huku kuingia katika ufalme ni lazima kutazamwe kama ni mwanzo tu wa wokovu wetu.

"Yesu akajibu, Amini, amini, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuuingia ufalme wa Mungu" (Yohana 3:5).

Huku kuingia katika Ufalme wa Mungu kulitolewa na Yesu Kristo na Kutimizwa kwa kutumia funguo za Ufalme zilizotolewa kwa Kanisa. Siku ya Pentekoste ilizindua Kanisa la Agano Jipya na Ujumbe uliohubiriwa siku ile ulifungua mlango wa kuingia katika Ufalme.

“Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na

Mitume wengine, tutendeje, ndugu zetu? Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" (Matendo 2:37-38).

Hiki kitabu kitachunguza namna ya kuingia katika ufalme.

FUNDISHO LA TOBA

SHARTI LA UKOMBOZI

"Ikiwa watu wangu, walioitwa kwa jina langu, watajinyenyekesha na kuomba na kunitafuta uso na kuziacha njia zao mbaya; basi nitasikia toka mbinguni, na kuwasamehe dhambi yao na kuiponya nchi yao" (2 Nyakati 7:14).

Nguvu zote za Mungu Mwenyezi kuwaokoa wanadamu waliopotea zinasubiri toba. Pasipo uamuzi wetu kuzikataa dhambi na kumfuata Bwana, mlango wa uzima wa milele umefungwa na nguvu ya mpango wa Mungu kwa ukombozi wetu haiwezi kufanya kazi.

Toba ni njia ya kunyakua neema ya Mungu kwa hali yetu ya upotevu. Kwa kutubu tunaupa upotevu kisogo na kuitazama neema ya mwokozi iliyo kuu.

Neema ya Mungu imetolewa kwa wote tunaonyesha ishara ya nia yetu kushiriki katika uokoaji wa Mungu wa mioyo yetu iliyopotea tunapogeuka toka dhambini. Mbali na kutokutamani adhabu yake, Yesu anataka kutuokoa kutokana na kushindwa kwetu.

"Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake kama wengine wanavyokudhani kukawia bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu yeyote apotee, bali wote waifikilie toba" (2 Petro 3:9).

Wokovu wetu tayari umeshatolewa; Ingawaje, haulazimishiwi mtu yoyote pasipo shauku na hiari yao. Kuingia katika Ufalme wa Mungu kuna rahisishwa kwa kutumia funguo za kwenye ufalme. Funguo hizi zilitumika kwa mara ya kwanza katika siku ya Pentekoste wakati Petro alipohubiri kwa makutano.

"Waliposikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro na Mitume wengine, tutendeje ndugu zetu? Petro akawaambia tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" (Matendo 2:37-38).

Kwa vile toba yenyewe haitoshi kutuokoa sisi, hatua muhimu ya kwanza katika safari ya kutoka katika Ufalme wa shetani na kuelekea Ufalme wa Mungu.

REHEMA YA AJABU

"Mtu huyo Mungu amemtukuza kwa mkono wake wa kuume awe mkuu na mwokozi awape waisraeli toba na msamaha wa dhambi" (Matendo 5:31).

"Waliposikia maneno haya wakanyamaza, wakamtukuza Mungu, wakisema Basi Mungu amewajalia hata mataifa nao toba liletayo Uzima" (Matendo 11:18).

Upendeleo wa toba si kitu tunachostahili. Si haki ambayo tunaweza kuidai kwa matakwa. Ni kwa kupitia neema ya Mungu iliyodhihirika tunaruhusiwa

kugeuka toka ile hali ya dhambi ya maisha yetu na kuwa wapokeaji wa Ukombozi. Israeli walipewa toba mataifa walipewa toba iletayo Uzima.

Kama haki ingetakiwa itendeke wote tungepotea pasipo tumaini lolote, pasipo fursa ya kugeuka toka katika dhambi zetu. Hii neema au Upendeleo wa Mungu tusiostahili wa kuturuhusu tutubu lazima ichukuliwe kama ni kuelezea pendo la Mungu lilivyo.

Kutazama toba kama ni jinsi ya kuepuka moto au wavu wa usalama kutuokoa sisi toka kucheza cheza na dhambi ni aibu kuu ya kudharau kusudi la Mungu katika kuruhusu toba.

Baadhi wamesema, unapofikiri sana mambo ya jinsi hiyo, kuwa watatubu tu watakapokuwa wanamtaka. Kufikiria neema ya Mungu kwa njia hiyo ni kama vile kucheza mchezo wa kipumbavu. Wakati rehema ya Mungu ni kubwa mno, hatuna uhakika kuwa toba itaruhusiwa katika hali za namna hiyo. Kama "tukiweka mkono wetu kulima" kutazama nyuma kunatufanya tusistahili. Tunapocheza na dhambi inayohadaa tusisahau wosia wa maandiko kwa "kumkumbuka mke wa Lutu" Toba ni lulu ya rehema ambayo hatutakiwi kuitupa mbele ya nguruwe.

MAHALI PA KUGEUKA

"Alipozingatia moyoni mwake alisema, Ni watumishi wangapi wa baba yangu wanaokula chakula na kusaza, na mimi hapa ninakufa kwa njaa. Nitaondoka nitakwenda kwa baba yangu na kumwambia, baba, nimekosa ..." (Luka 15:17-18).

Mfano wa mwana mpotevu ni kielelezo chenye nguvu na chenye kutia uchungu kabisa kwa toba ya kweli tunayoipata. Baada ya kuacha baraka na ulinzi wa nyumbani mwa baba yake, Yule kijana alichukua alichonacho na kukitapanya katika dhambi, pasipo na kosa, dhambi ni kitapanya maisha na mharibifu wa lile lililo jema. Njaa ilipokuja kama ilivyo wakati wote ambapo dhambi inatawala, hakupata rehema ulimwenguni.

"Hakuna mtu aliyempa" (Msitari wa 16). Katika hali hii ya kutisha na isiyo na tumaini, tamaa ya maganda aliyowalisha nayo nguruwe, mwana mpotevu hakuwa na la kufanya. Mshtuko wa ule mpasuko uliomfikia ulimrudisha katika fahamu zake, kama biblia isemavyo. "Alizingatia moyoni mwake". Hatua ya mwana mpotevu ya kutubu inatoa kielelezo kwa ajili yetu, hatua sahihi ya toba na kurejeshwa upya.

DALILI ZA TOBA

"Kwa sababu hiyo najichukia nafsi yangu na kutubu. Katika mavumbi na majivu" (Ayubu 42:6).

Udhilifu wa kukiri dhambi zetu, kukubali makosa yetu na kujitupa bila kuficha chochote mbele ya rehema ya Mungu ni kitendo cha kuvunjika. Kila hisia ya asili ya kiburi na kujihami ni lazima ishindwe na makadirio ya kweli yafanywe kwa hali yetu isiyo na tumaini. Ahadi ya 2 Nyakati 7:14 inaanza na, "Ikiwa watu wangu...watajinyenyekesha na kuomba".

Mwana mpotevu alijikuta katika uchungu wa kutisha. Kurudi nyumbani kwa baba yake kulimaanisha kukubali ujinga wake na kuwa radhi kukubaliana na chochote atakachokipata. Ametapanya sehemu ya haki yake kama mwana wa sasa

ilibidi aombe kuwa kama mtumishi. Pasipo na shaka pia alitambua asili ya ndugu yake mkubwa ya kutokusamehe na ilimpasa kukubali kwa kujitiisha yeye mwenyewe kwa dharau ya ndugu yake.

Ingawaje, kwa kuzingatia moyoni mwake mwana mpotevu alibeba lawama zote kwa makosa yake, na alikana kujitetea kokote. Utaalamu wa kisasa wa mambo ya akili mara nyingi hukimbilia chanzo kisicho na sababu yeyote cha kutupia lawama ili kuhamishia hatia kwa mtu mwingine.

Maana halisi ya neno toba ni "kugeuka," Kugeuka kabisa na kuanza mwelekeo mpya. Hii hatua ya kugeuka ni Mwanzo wa toba halisi.

"Maana huzuni iliyo kwa jinsi ya Mungu hufanya toba liletalo wokovu lisilo na majuto..." (2 Wakorintho 7:10).

"Huzuni ya toba ni kujuta kwa maovu yaliyofanywa, na kujutia miaka iliyopotezwa dhambini. Hii mara nyingi huongoza kwenye machozi ya upatanisho na mwokozi. Amani ambayo hufuata baada ya kumimina maumivu makali ya moyo mbele za Mungu ni baraka iliyoachiliwa hukumuni.

Hii haimaanishi kuwa toba ni kitendo cha kihisia tu. Uamuzi wa kuyageuza kikamilifu maisha ya mtu unahitaji kufikiri kwa makini na pia kwa mantiki. Baadhi wameonekana wakimwaga machozi ya maumivu halisi madhabahuni na bado wakashindwa kutimiza toba halisi. Huzuni ya Mungu iletayo toba katika mioyo yetu ni kujutia na kuacha machozi pasipo badiliko ni kuonyesha tu mateso ya mwenye dhambi ambaye hajatubu kabisa.

Huzuni halisi ya mwana mpotevu ilimwongoza kusema "Nitainuka na kwenda kwa baba yangu...".

"Zaeni matunda yapasayo toba..." (Luka 3:8).

Wakati mwingine hali za maisha hufanya marejesho kuonekana haiwezekani. Hatuwezi kurudisha miaka au kuondoa maumivu yaliyosababishwa na matendo yetu ya dhambi. Kwa upande mwingine kuna wakati mwingine makosa yanaweza kusahihishwa na toba ya kweli itatuongoza kwenye kulipa pale inapowezekana. Mwizi anayeendelea kufurahia utajiri wa wizi wake baada ya kumjia Mungu anahitajiwa kurudisha kile alichonyang'anya maongezi ya kudhuru yanatakiwa yafuatiwe na angalau kujaribu kujenga upya. Tabia njema iliyoharibika. Andiko linatuonyesha toba halisi ya Zakayo aliposema, "Nitarejesha...Ee Mungu uniumbie moyo safi, Uifanye upya roho iliyotulia ndani yangu" (Zaburi 51:10).

Kurudisha heshima hufuatia majuto na kulipa katika hatua ya toba. Moyo safi na roho iliyotulia hutupa nguvu kutembea juu katika mwanga wa uongaozi na mwelekeo wa Mungu. Kwa njia hiyo tunaweza kukamilisha mzunguko wa maisha mapya ambayo ni wokovu wetu, kwa sababu Kristo hakuja kuleta hukumu, ila kwamba Ulimwengu uokolewe katika Yeye. Mwana mpotevu pasipo shaka alitegemea karipio, ila badala yake alipata furaha kwa kurudi kwake. Vazi,viatu,pete na karamu vilikuwa ni mfano halisi wa maisha mapya tunayopata kwa njia ya muujiza wa toba.

"Pepo mchafu amtokapo mtu, hupitia mahali pasipo maji, akitafuta mahali pa kupumzika, asipate. Halafu husema, Nitarudi nyumbani kwangu nilikotoka; hata akija, aiona tupu, imefagiwa na kupambwa. Mara huenda akachukua pamoja naye pepo wengine saba walio waovu kuliko yeye mwenyewe, nao huingia na kukaa humo; na mtu yule hali yake ya mwisho huwa mbaya kuliko ya kwanza..." (Mathayo 12:43-45).

Utendaji wa toba umeelezwa hapa kwa uendeshaji wa aina tatu; Kuondoa dhambi; kutakasa; na kupamba. Toba halisi, hutakasa chombo na kuleta uzuri dhahiri na maendeleo kwenye maisha, Ingawaje, nguvu ya wokovu inatenda mengi zaidi ya hili. Hatua za kuzaliwa upya ni lazima ziendelee kwa kuleta maisha mapya na uwepo mpya ndani ya moyo uovu uliopita lazima badala yake uwakilishwe na haki ya maisha mapya. Roho ya Uovu ambayo imetolewa toka katika maisha ya mwenye dhambi lazima iwakilishwe na Roho Mtakatifu wa ahadi akili isiyotumiwa vizuri ni karaka na halisi ya shetani. Wokovu na kutembea na Mungu huwa havileti uvivu kwa mwamini.

"Tumieni kama akili ipasayo, wala msitende dhambi..." (1 Wakorintho 15:34).

Muamini mtendaji na aliyejazwa Roho hawezi kusumbuliwa na kuinuka kwa dhambi maishani mwake. Utupu ulioletwa na toba umekaliwa badala yake Roho wa Mungu na kazi ya haki.

ZAIDI YA TOBA ?

"Mkiangalia sana mtu asiipungukie neema ya Mungu..." (Waebrania 12:15).

Neno la Mungu kwa uhakika hutufundisha uhakika halisi wa ushindi wa kanisa juu ya dhambi. Ingawaje, haifundishi "Ukiokoka mara moja wakati wote umeokoka" au "Usalama wa milele" wa mwamini binafsi kwa kumaanisha kuwa haiwezekani kushindwa. Paulo alizungumza kuhusu kutokuibatilisha neema ya Mungu, na mstari hapo juu unasema kuhusu uwezekano wa kuipungukia neema ya Mungu.

"...alikataliwa maana hakuona nafasi ya kutubu, ijapokuwa aliitafuta sana kwa machozi" (Waebrania 12:17).

Huu mfano wa kukosa toba unaonekana katika maisha ya Esau. Anaitwa mtu wa ulimwengu, ambaye hakuthamanisha baraka za Mungu, ila aliziuza kwa starehe ya muda.

"...Iko dhambi iliyo ya mauti; sisemi ya kwamba ataomba kwa ajili ya hiyo" (Yohana 5:16).

Hatupewi ahadi ya upendeleo wa Mungu pasipo kujali matendo yetu. Ingawa neema ya Mungu ni nyingi mno, Inatolewa kwa mamlaka ya Mungu tu, na anaweza kuamua kuiondoa neema yake kutokana na mapenzi yake mwenyewe.

"Bwana akasema, Roho yangu haitashindana na mwanadamu..." (Mwanzo 6:3).

Suala la mwitikio wetu kwa Roho huonekana kuwa ndicho kipimo cha kuonyesha mwitikio wa Mungu kwetu. Kutokana na msamaha ulivyo, kuna muunganiko halisi. Katika sala ya Bwana tunaona uhusiano kati ya mapenzi yetu, kusamehe wengine na msamaha wa Mungu wa dhambi zetu. "Na utusamehe makosa yetu kama nasi tunavyowasamehe wanaotukosea." Pia inaonekana kuwa mtu asiyesamehe anaweza akawa na wakati mgumu kuamini kuwa atasamehewa. Kwa kiwango chochote, tunaona jinsi Bwana anavyojisikia kuhusu suala hilo katika habari ya wadeni wawili.

Yule aliyekataa kusamehe msamaha wake pia uliondolewa.

Tatizo halisi ni suala la kufanya moyo kuwa mgumu. Kwa kukataa mara kwa mara rehema za Mungu, tungeweza kujihukumu wenyewe kwa kupoteza usikivu wetu kwa Roho wake Mtakatifu. Huku kumzidisha Roho mara nyingi huongoza

kwenye kukosa uwezo wa kuguswa.

"Ambao wakiisha kufa ganzi wanajitia katika mambo ya ufisadi wapate kufanyiza kila namna ya uchafu kwa kutamani" (Waefeso 4:19).

"Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga na imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani; Kwa unafiki wa watu wasemao uongo, wakichomwa moto dhamira zao wenyewe" (1 Timotheo 4:1-2).

Kukataa kuenenda kwa Roho katika maisha yetu kutafanya mioyo yetu kuwa migumu kuisikiliza sauti yake. Pia itatoa fursa kwa roho nyingine zituongoze vibaya. Kumzimisha Roho wake kwa hakika kutatuongoza kwenye "Kufa ganzi" kama vile kanisa la Laudokia lilivyokua. Je? huku siyo kuelekea katika katika mwelekeo wa kumkufuru Roho Mtakatifu huzuia kabisa toba?

Kitu kinachothibitishwa katika maandiko haya ni uwezekano wa kupoteza fursa ya toba. Haisemi kuwa hii ni sheria. Watu wengi wameteseka kwa kuelewa vibaya maonyo haya kuhusu kumpinga Roho wa Mungu. Baadhi wamejihukumu wenyewe katika hali isiyo na tumaini kwa sababu walifanya dhambi baada ya toba yao ya mwanzo. Neema na rehema ya Mungu haiwezi kuzimwa na pia sisi hatuhitajiki kuvunjwa moyo. Soma hapa chini kipimo ambacho mtu anakataliwa na hivyo kukosa nafasi ya kutubu.

"Maana kama tukifanya dhambi kuhudi baada ya kuupokea ujuzi wa ile kweli, haibaki tena dhabibu kwa ajili ya dhambi" (Waebrania 10:26).

Kufanya dhambi kwa kukusudia huwa haimaanishi tu kufahamu kuwa kile tunachofanya ni kosa, ila kukusudia kwa kutafakari kabla ya kile kitendo na kutenda kwa kukusudia lile tendo. Mfano wa jambo hili ilikuwa ni kwa Akani, Ambaye hakupata rehema baada ya kupanga kwa kukusudia kutotii amri, hata kuandaa jinsi ya kufunika dhambi yake. Anania na Safira walikuwa na hatia ya tendo lile la kukusudia na kupanga jinsi ya kuficha. Toba ni sehemu inayoendelea na msamaha ni sehemu ya mpango wa Mungu wa wokovu wetu. Kinachofuata ni maana ya kimaandiko ya aina ya mtu aliyekataliwa toba.

"Mwaonaje? Haikumpasa adhabu iliyo kubwa zaidi mtu yule aliyemkanyaga mwana wa Mungu, na kuihesabu damu ya agano aliyotakaswa kwayo kuwa ni kitu ovyo na kumfanyia jeuri Roho wa Neema?" (Waebrania 10:29).

"Kwa maana hao waliokwisha kupewa nuru na kukionja kipawa cha mbinguni, na kufanywa washirika wa Roho Mtakatifu, na Kilionja neno zuri la Mungu na nguvu za zamani zijazo wakaanguka baada ya hayo, haiwezekani kuwafanya upya tena hata wakatubu; kwa kuwa wamsulubisha mwana wa Mungu mara ya pili kwa nafsi zao, na Kumfedheli kwa dhahiri" (Waebrania 6:4-6).

Neno la Mungu si jepesi kuhukumu Rehema ya Mungu haipotei kwa haraka kwa maana wale wanaojisikia wako chini ya hukumu, hujihisi kuhukumiwa kwa makosa yao, Yawapasa kuchukua faraja katika hisia zao. Kama tumekuwa wagumu mpaka kufa ganzi na hatusikii sauti ya Roho ikituonya juu ya dhambi na kutuita tutubu, basi tumepotea. Kama tukihisi Roho Anatuvuta tutubu, Basi asante Mungu

kwa nafasi ukengeufu ni zaidi ya kuanguka chini. Mungu anaturuhusu kutubu, anatusimamisha tena na kutusaidia kutembea pamoja naye.

TOBA NA WAKFU

Ili kueleza wazi jambo moja hebu tufananishe mambo mawili tofauti kati ya toba na Wakfu. Maana yake, toba ni kugeuka na kuanza upya mwelekeo mwingine. Inajumuisha kujitia kuishi maisha mapya yenye kuongozwa na Mungu. Wakfu kwa upande mwingine ni utoaji wa maeneo maalumu ya maisha yetu kwa Mungu na si lazima liwe ni suala linalohusu dhambi. Wakati toba inahusu mwanzo wa wokovu, wakfu inajumuisha kujitoa kwa kuendelea na hudumu. Wakati mwingine mtu anayemtafuta Mungu kwa mara ya kwanza anashindwa kuelewa hili jambo na hufikiri kwamba hajatubu mpaka ameweka wakfu kikamilifu maisha yake kwa Mungu wakfu kamili wakati mwingine ni jambo la miaka wakati toba inaweza kukamilishwa kwa mara moja. Kufikiri huku kumewaibia wengi furaha na maendeleo ambayo wangekuwa nayo katika Bwana. Watafutaji wa muda mrefu, wamechukua miaka kupokea kile Mungu angewapa katika muda mfupi. Karama za Mungu hazitolewi kwa misingi ya ukamilifu wetu, ila kama matokeo ya Imani yetu.

Toba inakamilishwa wakati ambapo hatupo kamili, kwa sababu ndiyo wokovu wetu. Wakfu ni hatua ya kufanywa kamili, na itabakia kuwa ni changamoto na uhitaji wa kila mwamini wa Mungu mpaka unyakuo.

UWEZA WA NGUVU ZA JINA LA YESU

"Jina la Bwana ni ngome imara; wenye haki hukimbilia, wakawa salama (Mithali 18:10).

Haiwezekani kuongeza zaidi nguvu iliyopo katika jina la Bwana. Hapana jina lingine kama hili.

"Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba" (Wafilipi 9-11).

Inaonekana kuwa upo uwezekano usio na mipaka wa matumizi ya jina la Bwana.

UPONYAJI

"Mtu wa kwenu amekuwa hawezi? na awaite wazee wa kanisa; nao wamwombee na kumpaka mafuta kwa jina la Bwana" (Yakobo 5:14).

"Lakini Petro akasema, mimi sina fedha, wala dhahabu, lakini nilichonacho ndicho nikupacho; kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, Simama uende" (Matendo 3:6).

"Jueni ninyi nyote na watu wote wa Israeli ya kuwa kwa jina la Yesu Kristo wa Nazareti, ambaye mlimsulubisha na Mungu akamfufua katika wafu, kwa jina

hilo mtu huyu anasimama alimzima mbele yenu" (Matendo 4:10).

KUTOA PEPO

"Akafanya hayo siku nyingi. Lakini Paulo akasikitika, akageuka akamwambia yule pepo, Nakuamuru kwa jina la Yesu Kristo, mtoke huyu. Akamtoka saa ile ile" (Matendo 16:18).

ISHARA NA MAAJABU

"...Na Ishara na maajabu vifanyike kwa jina la Mtumishi wako Mtakatifu Yesu" (Matendo 4:30b)

KUTOA SHUKRANI

"Na kumshukuru Mungu Baba siku zote kwa mambo yote katika jina lake Bwana wetu Yesu Kristo" (Efeso 5:20).

MAOMBI HUJIBIWA

"Nanyi mkiomba lolote kwa jina langu hilo nitafanya, ili Baba atukuzwe ndani ya mwana" (Yohana 14:13).

"...Amin Amin, nawaambia, mkimwomba Baba neno lolote atawapa kwa jina langu" (Yohana 16:23b).

UZIMA KWA JINA LAKE

"Lakini hizi zimeandikwa ili mpate kuamini ya kwamba Yesu ndiye Kristo, mwana wa Mungu; na kwa kuamini muwe na uzima kwa jina lake" (Yohana 20:31).

WOKOVU

"Naye atazaa mwana nawe utamwita jina lake Yesu, maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao" (Mathayo 1:21).

"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12).

KUHESABIWA HAKI

"Na baadhi yenu mlikuwa watu namna hii; lakini mlioshwa, lakini mlitakaswa, lakini mlihesabiwa haki, katika jina la Bwana Yesu kristo na katika Roho wa Mungu wetu" (1 Wakorintho 6:11).

KUOSHWA DHAMBI

"Basi sasa unakawilia nini? simama Ubatizwe, ukaoshe dhambi zako, ukiliitia jina lake" (Matendo 22:16).

ONDOLEO LA DHAMBI

"Huyo manabii wote humshuhudia, ya kwamba kwa jina lake kila amwaminiye atapata ondoleo la dhambi" (Matendo 10:43).

KUWA WANA WA MUNGU

"Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminio jina lake" (Yohana 1:12).

TUNATENDA KATIKA JINA LAKE

"Maana Mungu si dhalimu hata aisahau kazi yenu na pendo lile mlilolidhihirisha kwa jina lake, mmewahudumia watakatifu na hata hivi sasa mngali mkiwahudumia" (Waebrania 6:10).

"Na kila mfanyalo kwa neno au kwa tendo fanyeni yote katika jina la Bwana Yesu, mkimshukuru Mungu Baba kwa Yeye" (Wakolosai 3:17).

Mpaka uliowekwa tu juu ya jina la Bwana ni kuwa ni lazima litumike kutokana na neno la Bwana.

"...Kwa maana umeikuza ahadi yako kuliko jina lako lote" (Zaburi 138:2b).

Wana saba wa Skewa walijifunza kwa makosa yao kwa kulitumia jina la Bwana nje ya utaratibu wa neno lake haifai kitu.

"Baadhi ya Wayahudi wenye kutangatanga, nao ni wapunga pepo, wakajaribu kutaja jina la Bwana Yesu juu yao waliopagawa na pepo wachafu, wakisema, Nawaapisha kwa Yesu, yule anayehubiriwa na Paulo. Walikuwako wana saba wa mtu mmoja Skewa, Myahudi, kuhani mkuu, waliofanya hivyo. Yule pepo mchafu akawajibu akawaambia, Yesu namjua na Paulo namfahamu, lakini ninyi ni nani? na yule mtu aliyepagawa na pepo mchafu akawarukia wawili, akawaweza, akawashinda hata wakatoka mbio katika nyumba ile hali wa uchi na kujeruhiwa" (Matendo 19:13-16).

Wana wa Skewa hawakuwa na fursa ya kupata ushauri uliotolewa na Paulo kwa Timotheo.

"Lakini msingi wa Mungu ulio imara umesimama, wenye muhuri hii.Bwana anawajua walio wake. Na tena kila alitajae jina la Bwana na auache uovu" (2 Timotheo 2:10).

Kama unahitaji manufaa ya nguvu kubwa mno ya jina la Bwana, Basi lazima ulitumie ipasavyo kutokana na neno la Mungu.

Ni kweli ya hakika kuwa kulifuata Neno la Mungu ipasavyo ni muhimu kwa mambo yote. Watoto wa Eli walipotenda isivyopasa kwa sanduku la Agano, waliteseka, kama vile ilivyomtokea uza baadae. Hawa watu walikufa kwa sababu

walifahamishwa (au angalau walishajua) mpango wa Mungu ila waliamua kutenda kinyume.

"Lakini ijapokuwa sisi au malaika wa mbinguni atawahubiri ninyi Injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaaniwe" (Wagalatia 1:8-9).

Kwa hakika si jambo dogo kutumia vibaya vitu vya Mungu. Kuna thamani ya kutumia kila wakati na nguvu inayohitajika kutafuta waziwazi kile neno la Mungu linavyosema.

"Angalieni mtu asiwafanye mateka kwa elimu yake ya bure na madanganyo matupu, kwa jinsi ya mapokeo ya wanadamu, kwa jinsi ya mafundisho ya awali ya ulimwengu, wala si kwa jinsi ya Kristo" (Wakolosai 2:8).

Katika yafuatayo ninataka nitazame mambo kadhaa ya jina la Bwana na kufuata kwa kupitia Neno la Mungu kuona umuhimu wa kuogofya wa mambo ya kila mmoja wetu sisi.

JINA LA YESU KATIKA KANISA LA KWANZA

Mtazamo kaika Agano Jipya na hasa katika kitabu cha matendo hufunua kuwa jina la Yesu lilikuwa ni kiini cha kati katika kufikiri na kuhubiri kuwa mitume.

"Lakini walipomwamini Filipo akizihubiri habari njema Ufalme wa Mungu na jina lake Yesu wakabatizwa, wanaume na wanawake" (Matendo 8:12).

"Akawaambia ndivyo ilivyoandikwa, kwamba kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi, kuanza tangu Yerusalemu" (Luka 24:46).

Ilikuwa ni sahihi kabisa sehemu iliyo hifadhiwa sana Imani yao ni mtazamo wa mateso waliyovumilia kwa kulihubiri jina la Yesu.

"Mkilaumiwa kwa ajili ya jina la Kristo ni heri yenu; kwa kuwa Roho wa utukufu na wa Mungu anawakalia" (1 Petro 4:14).

"Sisi tumeona vema, hali tunapatana kwa moyo mmoja, kuwachagua watu na kuwapeleka kwenu pamoja na wapendwa wetu Barnaba na Paulo. Watu waliohatarisha maisha yao kwa ajili ya jina la Bwana wetu Yesu kristo" (Matendo 15:25-26).

"Ndipo Paulo alipojibu, mnafanya nini kulia na kunivunja moyo? kwa maana mimi licha ya kufungwa, ni tayari hata kuuawa. katika Yerusalemu kwa ajili ya jina lake Bwana Yesu" (Matendo 21:13).

Fundisho la jina la Yesu lazima lilionekana la muhimu katika kanisa kwanza kama pasiposababu nyingine kuliko mateso dhabiti kinyume chake.

"Lakini neno hili lisije likaenea katika watu na tuwatishe wasiseme tena na mtu awaye yote kwa jina hili" wakawatia, wakawaamuru wasiseme kabisa wala kufundisha kwa jina la Yesu" (Matendo 4:17-18).

"Wakakubali maneno yake; nao walipowaita mitume, akawapiga, wakawaamuru wasinene kwa jina lake Yesu; kisha wakawaacha waende zao" (Matendo 5:40).

“Kweli, mimi mwenyewe naliona ndani ya nafsi yangu kwamba yanipasa kutenda mambo mengi yaliyopingamana na jina lake Yesu Mnazareti” (Matendo 26:9).

Shetani hajali kama tuna kanisa. Atahudhuria kama akiruhusiwa. Kitu

shetani anachokijali ni kuwa tusiwe na nguvu za Mungu na kweli halisi katika makanisa yetu. Haya mambo atapigana nayo. Sanhedrini (baraza la Kiyahudi) hawakujali sana kuhusu uponyaji na miujiza ile mitume waliyoitenda, lakini waliwapinga sana kwa kutenda haya mambo katika jina la Yesu, na kujaribu kuwazuia mitume kufundisha katika jina lile.

Kwa karne nyingi toka wakati ule, shetani hajaacha kupambana kinyume cha fundhisho la mitume kuhusu jina la Yesu. Anatambua kuwa kuna nguvu nyingi na mamlaka hapo. Tuwe waangalifu tusije tukapotezwa kwa filosofia na mafundisho ya wanadamu.

"Nao waniabudu bure, wakifundhisha mafundisho yaliyo ya wanadamu" (Mathayo 15:9).

Nakubali kuwa kama tutashika maoni ya wanadamu haijalishi heshima na wadhifa wao, kama ndilo fundisho la kwanza la uwazi la neno la Mungu, basi hatuna tofauti yoyote na Mafarisayo.

FUNDISHO LA MITUME

"Mmejengwa juu ya msingi wa mitume na manabii, naye Kristo Yesu mwenyewe ni jiwe kuu la pembeni" (Waefeso 2:20).

Tena ni muhimu kubaki ndani ya mipaka ya maandiko. Ninaweza kuvuvuwa na kuinuliwa na maneno ya mtu mwingine ila naweza tu kuokolewa katika upotevu wangu kwa neno la Mungu lililobadilika.

"Lakini watu wabaya na wadanganyaji wataendelea na kuzidi kuwa waovu, wakidanganya na kudanganyika. Bali wewe ukae katika mambo yale uliyofundishwa na kuhakikishwa kwa maana unajua ni akina nani ambao ulijifunza kwao, na ya kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika kristo Yesu. Kila andiko, lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuonya watu makosa yao na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema" (2 Timotheo 3:13-17).

"Nasi tuna lile neno la unabii lililo Imara zaidi ambalo, mkiliangalia, kama taa ing'aayo mahali penye giza. Mwafanya vema, mpaka kutakapopambazuka na nyota ya asubuhi kuzuka miyoyoni mwenu. Mkijua neno hili kwanza ya kwamba hakuna unabii katika maandiko upatao kufasiriwa kama apendavyo mtu fulani tu. Maana unabii haukuletwa popote kwa mapenzi ya mwanadamu; bali wanadamu walinena yaliyotoka kwa Mungu, wakiongozwa na Roho Mtakatifu" (2 Petro 1:19-21).

Kwa hasara ya kuonekana kulitenda kazi, jambo hili maandiko hapo juu yamejumuishwa kuhusu umuhimu wa wazi wa kuwa na mwelekeo wa Neno la Mungu kwa ajili ya Wokovu wetu. Hapo mwanzo ilinenwa, mtu aliyedai kuzaliwa mara ya pili, kwa maandiko mengine hasa kitabu cha matendo ya mitume, Vilikuwa si vya kutumainiwa. Hii inaweza ikawa kweli kwa sababu katika kanisa la Kwanza hawakutambua mpango halisi wa Mungu. Kutokana na fikra ya aina hii, ilikuwa ni mpaka baadaye ambapo watu kama "Mababa wa kanisa" waliweza kwa kupitia elimu ya juu na akili kutuletea Ufahamu halisi. Nashangaa kwa nini Yesu hakuwatafuta watu kama hao hapo mwanzo, na kuwapa Injili mikononi mwao? Mitume waliitwa na wayahudi kuwa wajinga na wasio na elimu ila walichukua Ufahamu wa wale waliokuwa na Yesu. Kwa hakika huu ulikuwa ni mpango wa

Mungu,kwa sababu kama maandiko yasemavyo, Mungu amewachagua wanyonge wapumbavu, na kadhalika. Kufanya kazi yake ili kwamba yeye apokee utukufu. Mtume Msomi Paulo hakuwapinga Mitume wengine kwa ajili ya ujumbe wao wala hakuwatendea wema kwa kujaribu kurekebisha mafundisho yao. Ukweli ni kuwa haihitajiki elimu ya juu sana kuelewa na kufuata njia ile "Msafiri, ingawaje ni mpumbavu, hawezi kupotea ndani yake" Ilikuwa ni baadaye ambapo wanadamu walidhubutu kuchukua sehemu ambayo mtu wa kawaida asingeweza kutambua na kufuata mafundisho ya Mungu. Ilikuwa ndio wakati hawa wataalamu walipoanza kuchanganya mawazo yao katika mafundisho ya neno la Mungu ndipo kanisa likapotoka kutoka ujumbe rahisi wa Mitume.

Hushangaza kwa ujasiri wa yeyote yule ambae hakuthubutu kudharau fundhisho halisi la Neno la Mungu, kama kitabu cha Matendo hakiwezi kuaminika basi tunaweza kuamini lolote la Agano Jipya? Kila mmoja wao wa waandishi wa Agano Jipya alijumuishwa katika kitabu cha matendo. Hakuna hata mmoja wao aliyebishana nacho. Hakuna mmoja wao aliyedharau mafundisho katika kitabu cha Matendo. Hakuna mahali palipotajwa katika Neno la Mungu kuwa kuna uhitaji wa kuurekebisha ujumbe wa Mitume. Badala yake, Neno la Mungu linasema kuwa tunapaswa kuutulimia pamoja na unabii kama msingi wa Imani, Na Yesu Kristo akiwa jiwe kuu la Pembeni.

Unaposikia ujumbe uliopita katika vinywa vya watu wengi, Inawezekana kabisa ule ujumbe ukapoteza maana yake. Ili kuwa na imani iliyopewa watakatifu mara moja tu, tunahitajika kwenda moja kwa moja kwenye chanzo, hicho ni neno la Mungu. Utoaji safi wa fundisho lolote unatakiwa uanzie katika chanzo chake. ambapo wanajisi wa maoni na wenye upendeleo hawajaingia ndani. Hebu sasa tuwatazame mitume.

"Ndipo akawafunulia akili zao wapate kuelewa na maandiko..." (Luka 24:45).

Angalia hapa mitume walipewa ufahamu dhahiri wa maandiko na Yesu mwenyewe.

"Akawaambia ndivyo ilivyoandikwa, kwamba Kristo atateswa na kufufuka siku ya tatu; na kwamba mataifa yote watahubiriwa kwa jina lake habari ya toba na ondoleo la dhambi kuanza tangu Yerusalemu" (Luka 24:46-47).

Mitume waliamriwa na Yesu kwenda Yerusalemu na kungoja mpaka wapokee nguvu toka juu (Luka 24:49). Walifanya hivi kwa furaha. Yesu aliwaambia kuwa wangepokea nguvu badala ya Roho Mtakatifu kuwajilia juu yao, na kuwa wangekuwa mashahidi wake katika Yudea, Samaria, na dunia nzima (Matendo 1:8). Mlango wa pili wa Matendo unaanza na ile ahadi kutimizwa katika hali ya ajabu. Kwa mvumo wa upepo uendao kwa kasi. Roho alijaza sehemu wazi za nafsi zao. Mara wakaanza kunena kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka. Tukio hili liliposikika maelfu walikuja wakikimbia na kushangaa, wakimpa mtume Petro nafasi kwa ujumbe wa kwanza uliohubiriwa katika kanisa la Agano Jipya. Hili ni mojawapo ya tukio muhimu sana katika mpango wa Mungu kwa kuhubiri Injili, Ilitanguliwa na upepo uvumao na moto ukawavuta wasikilizaji maelfu, je, tuamini kuwa Mungu angemruhusu Petro kutangaza ujumbe potovu? Kwa hakika kazi za huduma ya Yesu, dhabihu ya Kalvari, muujiza wa Ufunuo visingewakilishwa na mtume ambaye hakufanya kazi yake aliyoachiwa! Ingawaje Petro alihubiri kwa nguvu na upako ambao uliwagusa maelfu na kuuliza, "Tutendeje ndugu zetu?", je, akikosa uwezo wa kuwaambia njia ya wokovu pamoja na ukweli kuwa Yesu

alimwambia kuwa angempa funguo za kwenye Ufalme wa mbinguni, Je Petro hakuwa na ujumbe sahihi wa kuhubiri siku ile? Ninaafiki kuwa Petro alikuwa ana ujumbe, na hata mamlaka ya Uungu na upako wa kuhubiri. Ule ujumbe unaobakia hivi leo kama sehemu ya msingi wa kanisa na hatuthubutu kupuuza kama wengine walivyofanya. Jibu la Petro kwa Swali "Tufanye nini?" Linapatikana katika Matendo 2:38-39.

"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi matapokea kiwapa cha Rohoa Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie" (Matendo 2:38-39).

Mkutano wa Wahayudi watauwa kutoka katika kila taifa chini ya mbingu hawakufanya ghasia ili wapate maelekezo ya uwazi, ila walitii mara moja!

Tunapofuatana na kitabu cha matendo, tutaona kuwa mara kwa mara ujumbe wa nguvu ya Jina la Yesu kwa Uponyaji, wokovu na kadhalika ulihubiriwa kikamilifu na mitume na pia kuthibitishwa kikamilifu na nguvu za Mungu. Kwa nini hatusikii ujumbe huu ukihubiriwa katika jamii nyingi za kikristo leo? Ni mapenzi ya Mungu huu ujumbe unyamazishwe katika makanisa yetu? Au adui yetu shetani ameuleta huu ukimya kwa kuweka badala yake falsafa na mapokezi na mapokeo mahali pa Fundisho la mitume?

Katika sura ya wa tatu wa Matendo tunaona Petro na Yohana wamewafarakisha katika utata kuhusu uponyaji wa yule kiwete. Wakiwa hawana fedha na dhahabu walimpa yule mwombaji walichokua nacho. "Katika jina la Yesu Kristo wa Nazareti Simama na uende." Ghasia zalizofuatia kuuzunguka huu upanyaji ulielekezwa kwenye swali moja; Ni kwa jina la nani uponyaji ulifanywa? Jibu la Petro katika (Matendo 4:11-12).

"Yeye ndiye jiwe lile lililodharauliwa na ninyi waashi, nalo limewekwa kuwa jiwe kuu la pembeni. Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:11-12).

Mwitikio wa wengi kwa yote haya ingekuwa; "Ndiyo kwa hakika hatulikani jina la Bwana Yesu katika kanisa letu. Tunaombea wagonjwa katika jina la Yesu, tunatoa pepo katika jina la Yesu, tunaomba kwa jina lake, na kadhalika. Hii ni hakika kama inavyotakiwa iwe. Hata hivyo ngoja nionyeshe sehemu moja ya muhimu sana ambapo jina la Yesu limefungiwa nje na wengi.

UBATIZO KATIKA JINA LA YESU KRISTO

Hebu turudi katika siku ya Pentekoste, ambayo ni siku ya kuzaliwa kanisa. Katika siku Roho Mungu alimiminwa kwa mara ya kwanza katika historia kulipa kanisa nguvu ambayo haikupewa wanadamu kabla. Kama vile maelfu walikusanyika na kuuliza "Jambo hili maana yake ni nini?" Petro akasogea mbele kumhubiri Yesu. Baada ya kutangaza kuwa Yesu alikuwa ni masihi wao, Roho wa Mungu alitembea kwa ushawishi mkubwa akiwahimiza mkutano kupiga kelele, "Tutendeje ndugu zetu?" Ndipo Petro pamoja na mashahidi kama 120 pamoja na mitume wengine wote, waliendelea kuwaonyesha mkutano njia ya wokovu.

"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu

Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie" (Matendo 2:38-39).

Lililonukuliwa hapo juu ni Neno la Mungu linatuambia kuwa yatupasa kubatizwa katika jina la Bwana Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zetu. Pia inasema kuwa ahadi ya ondoleo la dhambi na kujazwa na Roho mtakatifu ni kwa wote. Yote haya yamenenwa kwa maneno dhahiri kabisa, na kama sehemu ya neno la Mungu, lazima lihubiriwe kila mahali ambapo Neno la Mungu linatangazwa. Hata hivyo kuna wale wanakana umuhimu wa ubatizo, wakifanya mapokeo yasiyo na nguvu kuliko sehemu muhimu ya ubatizo, kuzaliwa upya. Ni muhimu kwetu kudhibitisha kwa andiko sehemu muhimu ya ubatizo unaotenda katika wokovu wetu.

WOKOVU KATIKA JINA

"Yesu akajibu, Amin Amin, nakuambia, Mtu asipozaliwa kwa maji na Roho hawezi kuingia ufalme wa Mungu" (Yohana 3:5).

Yesu alisema hivyo Je tupunguze? Je, hakuna uhusiano wa wazi kabisa kati ya kuzaliwa kwa maji na ubatizo? Vipi kuhusu suala la kuzaliwa kwa Roho? Je, kupokea kipawa cha Roho Mtakatifu, hakutimizi hitaji hilo?

"Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulibatizwa pamoja naye kwa njia ya Ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama tulivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika tutaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake" (Warumi 6:3-5).

Katika yeye mmetahiriwa kwa tohara isiyofanyika kwa mikono, kwa kuuvua mwili wa nyama kwa tohara ya Kristo. Mkazikwa pamoja naye, kwa kuziamini nguvu za Mungu aliyemfufua katika wafu. Na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye akisha kutusamehe makosa yote" (Wakolosai 2:11-13).

Tunaona kutoka katika maandiko hapo juu kuwa vyote msamaha wa dhambi na nguvu ya ufufuo pasipo na mashaka vimehusishwa na ubatizo. Pia ni kweli kuwa katika kanuni ya tohara, mtoto aliyezaliwa anapata jina lake. Kwa asili hufuata huo ubatizo, ambao ni tohara ya Agano Jipya, tukichukua juu yetu jina la Yesu.

Kuongezea hili, desturi ya Biblia ya mke huchukua jina la Mumewe; katika mifano yote miwili ule wa Tohara wa mtoto wa Mungu, na pia kuwa bibi arusi wa Kristo, tunachukua jina lake. Kama hukulipokea katika ubatizo, ulilipokea wapi? "Hawalitukani jina lile zuri mliloitwa?" (Yakobo 2:7).

"Simeoni ametueleza jinsi Mungu hapo kwanza alivyowaangalia mataifa ili achague watu katika hao kwa ajili ya jina lake" (Matendo 15:14).

Inaonekana kuwa hii inaelezea wale ambao wamekataliwa na Kristo, ingawaje wamefanya uponyaji wa miujiza hata kutoa pepo kwa jina lake. Ingawaje walilitumia jina la Yesu, hawakuitwa kwa jina la Yesu. Ni suala la utambulisho.

"Si kila mtu aniambiaye Bwana, Bwana atakayeingia katika ufalme wa mbinguni bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni. Wengi wataniambia siku ile Bwana, Bwana, hatukufanya unabii kwa jina lako, na kwa jina lako kutoa pepo, na kwa jina lako kufanya miujiza mingi? Ndipo nitawaambia dhahiri, siwajui ninyi kamwe; Ondokeni kwangu, ninyi mtendao maovu" (Mathayo 7:21-23).

Yatupasa tukumbuke kuwa wanafunzi walitenda miujiza, kutoa pepo n.k. Kabla hawajapokea jina la Yesu katika Ubatizo. Mwanadamu wa pekee asiye na dhambi aliyewahi kuishi na Yesu Kristo. Alivumilia msalaba, mashtaka ya uongo, mapigo na manyanyaso ili ashirikishwe dhambi zetu.

"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye" (2 Wakorintho 5:21).

"Hakika ameyachukua masikitiko yetu, Amejitwika huzuni zetu; lakini tulimdhania ya kuwa amepigwa, Amepigwa na Mungu, na kuteswa. Bali aliyeruhiwa kwa makosa yetu, Alichubuliwa kwa maovu yetu; Adhabu ya amani yetu ilikwa juu yake. Na kwa kupigwa kwake sisi tumepona. Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe. Na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote" (Isaya 53:4-6).

Chini ya Sheria mwenye dhambi aliweka mkono wake juu ya kichwa cha dhabibu na kuungama dhambi zake. Mwana kondoo alifungamanishwa na dhambi za yule mtu, na aliuwawa. Haishangazi Yohana mbatizaji alipiga kelele "Tazama mwana kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya Ulimwengu." Yesu alikuwa mwana kondoo wetu wa kutolewa dhabihu, Ingawaje hakuwa na dhambi, alifungamanishwa na dhambi zetu. Kwa njia ya Ubatizo, tunaunganishwa na utakatifu Wake kwa njia ya Ubatizo, tunaitwa kwa jina la Yesu.

NJIA ZA WOKOVU

"Watu wasiotii hapo zamani uvumilivu wa Mungu ulipokuwa ukingoja, siku za Nuhu, Safina ilipokuwa ikitengenezwa; ambamo ndani yake wachache, yaani watu wanane, waliokoka kwa maji. Mfano wa mambo hayo ni Ubatizo, unaowaokoa ninyi pia siku hizi? (Siyo kuwekea mbali uchafu wa mwili, bali jibu la dhamiri safi mbele za Mungu), kwa kufufuka kwake Yesu Kristo" (1 Petro 3:20-21).

Hapa Petro anaeleza mfano wa jinsi Nuhu na Jamaa yake waliokolewa kwa maji. Akasema tena," Ubatizo unatuokoa pia siku hizi."

"Na watu wote na watoza ushuru waliposikia hayo, waliikiri haki ya Mungu, kwa kuwa wamebatizwa kwa ubatizo wa Yohana. Lakini mafarisayo na wanasheria walilipinga shauri la Mungu juu yao, kwa kuwa hawakubatizwa naye" (Luka 7:29-30).

Kukataa ubatizo ni kukataa shauri la Mungu. Tafadhali elewa kuwa ni wanasheria waliokataa Ubatizo. Watu hawa ni wale walio waangalifu wa kutokufanya jambo lolote zaidi ya wanavyofikiri ni muhimu kabisa katika Ufalme wa Mungu roho hii ni pinzani moja kwa mojana bibi arusi.. Yesu alisema "Aaminiye na kubatizwa ataokoka..." (Marko 16:16a).

Kwa kutumia mwanga wa ushahidi mwingi wa kimaandiko lazima tujue kuwa Ubatizo ni muhimu kupita kiasi. Kama haikuwa ni muhimu kwa nini/basi Yesu aliamuru? Mathayo 28:19 (Matendo 2:38 & Matendo 10:48). Kwa nini Paulo na

Sila walimbatiza mkuu wa gereza wa Filipi usiku wa manane? Kwa nini Mitume waliutii? (Matendo 16:33). Kwa nini Paulo aliwabatiza kwa mara ya pili wanafunzi wa Yohana mbatizaji wa Efeso katika jina la Yesu? (Matendo 19:4-5).

Tumesikia kuwa Ubatizo ni "ishara ya nje ya kazi ya ndani ya neema". Mtu yeyote anaweza kutafuta andiko lenye kuunga mkono tamko hilo?

Kuna wale watakaosema kuwa tunafundisha wokovu kwa matendo. Hakuna mtu awezaye kuokolewa kwa matendo peke yake.

"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya Imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo, mtu awaye yote asije akajisifu" (Waefeso 2:8-9).

Niruhusu nionyeshe mifano miwili ya muhimu sana ya wazo hili: nikiwataja Nuhu na Ibrahimu.

"Lakini Nuhu akapata neema machoni pa Bwana" (Mwanzo 6:8).

"Maana maandiko yasemaje? Ibrahimu alimwamini Mungu, Ikahesabiwa kwake kuwa haki" (Warumi 4:3).

Muujiza wa neema iliyosababisha wokovu katika maisha ya hawa watu ni ushahidi halisi ndani ya maandiko. Nuhu alipata kibali machoni pa Bwana. Ndiyo sababu aliokolewa kwa sababu ya ile neema alipewa mpango wa wokovu ambao aliutii. Hivyo ndivyo alivyookolewa. Pasipo kibali cha Mungu ingekuwa haina maana kwa Nuhu kujenga Safina. Lile tendo pekee lisingeweza kumwokoa. Ingawaje, pamoja na kupewa neema ya Mungu, Imani ya Nuhu na Utii kwa mpango wa Mungu wa wokovu ulimkomboa kutokana na gadhabu. Hapana, hatuwezi kuokolewa pasipo utii.

"Basi wapendwa wangu, kama vile mlivyotii siku zote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka. Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu, kutaka kwenu kutenda kwenu, kwa kutimiza kusudi lake jema" (Wafilipi 2:12-13).

Ibrahimu alimwamini Mungu kwake ikahesabiwa kuwa haki. Tunawezaje kujua kuwa alimwamini Mungu? Kwa sababu alipopokea mwito wa Bwana, alitii, Ni jambo lisilo la maana kubisha kuwa huenda mtu ameokolewa kwa Imani au kwa matendo, kwa sababu Biblia inatuambia hatuwezi kuokolewa kwa matendo, na kuwa Imani pasipo matendo imekufa, ikiwa pekee. Imani na matendo zinaungana pamoja na kuumba utii ambao mwishowe ni wokovu wetu.

"Maana ninyi nyote mliobatizwa katika Kristo mmemvaa Kristo. Na kama ninyi ni wa Kristo, basi, mmekuwa Uzao wa Ibrahimu, na warithi sawasawa na ahadi" (Wagalatia 3:27, 29).

Yesu akasema, "Mkinipenda mtazishika amri zangu." Pia 2 Wathesalonike 1:8, inaeleza kuwa Mungu atalipa kisasi kwa wale wasiotii Injili ya Yesu Kristo. Waebrania 5:9 inatangaza kuwa Yesu ni mwanzilishi wa wokovu wa milele kwa wote wanaomtii kwa hiyo Neno la Mungu linapotuamuru tubatizwe, tunaweza kuokolewa tusipotii?

HAPANA JINA JINGINE

"Yesu akaja kwao akasema nao, akawaambia Nimepewa mamlaka yote mbinguni na duniani. Basi enendeni, mkawafanye mataifa yote kuwa wanafunzi,

mkiwabatiza kwa jina la Baba na Mwana na Roho Mtakatifu; na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote hata ukamilifu wa dahari" (Mathayo 28:18-20).

"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" (Matendo 2:38).

"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12).

Tunasoma katika Injili kuwa Yesu aliwaamuru mitume wake kufundisha na kubatiza. Amri hii ilitolewa na Yesu katika kufunga huduma yake, kabla tu ya kupaa kwenda mbinguni. Kanuni pekee ya ubatizo iliyotumika katika Mathayo, Marko, Luka na Yohana ni ile ya Yohana mbatizaji. Mwitikio wa mitume kwa amri ya Yesu unapatikana katika kitabu cha Matendo.

"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate Ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu" (Matendo 2:38).

Utii wa Petro kwa amri ya Yesu katika Mathayo 28:19 ilikuwa ni kuwaamuru watu kubatizwa katika jina la Yesu.

"Lakini walipomwamini Filipo, akizihubiri habari njema za Ufalme wa Mungu, na jina lake Yesu Kristo, Wakabatizwa wanaume na wanawake" (Matendo 8:12).

"Na Mitume waliokuwako Yerusalemu waliposikia ya kwamba Samaria imekubali neno la Mungu, wakawapelekea Petro na Yohana; ambao waliposhuka wakawa ombea wakampokee Roho mtakatifu; kwa maana bado hajawashukia hata mmoja wao, ila wamebatizwa tu kwa jina lake Bwana Yesu" (Matendo 8:14-16).

Filipo aliwabatiza waongofu wa Samaria katika jina la Yesu, Ubatizo huu ulitambuliwa na Petro na Yohana, ambapo baadae waliwaombea watu ili kwamba wapokee Roho Mtakatifu.

"Akaamuru lile gari lisimame; wakatelemka wote wawili majini, Filipo na Yule towashi; naye akambatiza" (Matendo 8:38).

Hili tukio la Ubatizo halituelezi ni kanuni gani iliyotumika isipokuwa ilifanyika kwa kuzamisha. Towashi wa Kushi (Ethiopia) aliendelea na safari yake akifurahi na Filipo alinyakuliwa na Roho wa Bwana. Kweli mbili hapa zitaonyesha mwishowe kuwa Filipo alimbatiza mwithopia katika jina la Yesu; kwanza kuwa Filipo hapo awali alibatiza akitumia jina la Yesu tunatambua kutokana na matendo 8:16; Pili imetambulikana kuwa namna ya kimapokeo ya kumbatiza mwi-Ethopia ni katika jina la Yesu, na kuwa hili lilikuwa ni kutokana na ushuhuda wa Towashi wa Ethopia. Kama ushuhuda huo ni kweli, basi ni mantiki kudhani kuwa Filipo alimbatiza kwa kutumia jina la Yesu. Hatuitegemei taarifa hii ingawaje kama kumbukumbu ya kimaandiko inatosha kufahamu kweli.

"Mara vikaanguka machoni pake vitu kama magamba, akapata kuona akasimama akabatizwa" (Matendo 9:18).

Hakutaja aina ya ubatizo katika tukio la ubatizo wa Sauli, ingawaje tunatambua kutokana na tukio lililofuata la ubatizo wa mara ya pili wa wanafunzi wa Efeso wa Yohana mbatizaji, kuwa Paulo aliwaamuru wabatizwe katika jina jina la Bwana Yesu. Inaonyesha kuwa kwa jinsi iyo hiyo.

"...Ndipo Petro akajibu, Ni nani awezaye kukataza maji, hawa wasibatizwe, watu waliompokea Roho Mtakatifu, vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo. Ndipo wakamsihi azidi kukaa siku kadha wa kadha" (Matendo 10:46-48).

Nyumba ya Karnelio iliamriwa kubatizwa katika jina la Bwana. Mitume tayari walishakiri Yesu kuwa ni mwokozi wao. Pia, ilikuwa ni Petro aliyewaamuru wabatizwe katika jina la Yesu Kristo siku ile ya Pentekoste Tunachukilia kuwa hakubadilisha ujumbe wake kati ya Matendo 2 na Matendo 10.

"Akawakaribisha saa ile ile ya usiku, akawaosha mapigo yao, kisha akabatizwa yeye na watu wake wote wakati huo huo" (Matendo 16:33).

Hakuna kutajwa kokote kwa kanuni ya ubatizo mahali hapa. Ingawaje, tunajua kuwa ni Paulo aliyehudumu katika hali hii, na kumbukumbu pekee tuliyonayo ya Paulo kuamuru ubatizo inahusisha ubatizo katika jina la Yesu.

"Akawauliza, Basi mlibatizwa kwa ubatizo gani? Wakasema kwa ubatizo wa Yohana. Paulo akasema, Yohana alibatizwa kwa ubatizo toba, akiwaambia watu wamwamini yeye atakayekuja nyuma yake, yaani Yesu. Waliposikia haya wakabatizwa kwa jina la Bwana Yesu" (Matendo 19:3-5).

Paulo aliwaza kuwa kama hawa wanafunzi hawakuwahi kusikia kuhusu kipawa chaRoho Mtakatifu, Pia hawajawahi kusikia kuhusu Yesu. Mahubiri ya mtume wakati wote yalimtangaza Yesu kuwa ni kristo. Mahubiri yao yalifuatana na kumwagwa kwa Roho Mtakatifu. Mahubiri yao yalijumuisha fundisho la ubatizo pia. Wakati hawa wanafunzi walikuwa hawajasikia kuhusu kupokea Roho Mtakatifu Paulo mara moja akawauliza jinsi walivyobatizwa. Kwa kuwa hawakujua lolote kuhusu ubatizo mwingine isipokuwa ule wa Yohana mbatizaji, Paulo alijua kuwa hawajawahi kusikia Injili, akawahubiria kuhusu Yesu. Walipoipokea hili fundisho moja kwa moja akawabatiza katika jina la Yesu na kuwawekea mikono ili kwamba wampokee Roho Mtakatifu. Walimpokea kwa ishara ya kunena kwa lugha. Paulo pasipo shaka aliweka umuhimu juu ya ubatizo, ambayo inashuhudiwa kwa ile hakika kuwa aliwabatiza wanafunzi huko Efeso mara nyingine tena katika njia aliyohisi kuwa ni sahihi, na pia kutokana na hakika kuwa alijisumbua kubatiza nyumba ya mkuu wa gereza wa Filipi katikati ya usiku. Paulo hakuwa na maongezi yeyote mabaya kuhusu kumtambua Bwana wake. Hili tatizo lilitatuliwa milele alipokuwa akienda Dameski mara aliuliza, "U nani wewe, Bwana?" Jibu, "Mimi ni Yesu" aliondoka pasipo na shaka katika ufahamu wake.

Nyaraka ni barua zilizoandikwa kwa makanisa yaliyoanzishwa tayari. Siyo maelezo ya kihistoria na hazina maelezo ya wokovu au mabatizo. Kwa hiyo, kumbukumbu pekee tulizonazo kuhusu mabatizo kufuatia amri ya kristo ni matukio saba yaliyohifadhiwa katika kitabu cha Matendo.

Kama tulivyokwisha kuonyesha katika kila jambo kati ya haya moja ya mambo mawili yanatokea: 1) Kanuni ya Ubatizo kwa kutaja jina la Yesu inatumika, au, 2) Ubatizo unaongozwa kwa mtu anayeweza kuonyeshwa kuliamini na kufanya ubatizo katika jina la Yesu.

Hakuna mfano mwingine wa ki-Biblia uliotolewa. Hakuna hata mara moja tunapopata kutajwa katika maandiko wa mtu yeyote kubatizwa kwa kutumia kanuni nyingine yoyote.

Wengi wamebishana kuhusu tendo la ubatizo "Katika jina la Baba na Mwana, na Roho Mtakatifu" wakionyesha Mathayo 28:19 kama amri kwa kufikia mtazamo

huu, ni muhimu kwetu sisi kukumbuka kuwa Yesu hakuwa anabatiza aliposema maneno haya. Badala yake alikuwa anatoa maelekezo kwa wanafunzi wake. hakuna hata mara moja katika Neno la Mungu ambapo panaweza kuonyeshwa au hata panapofahamisha kuwa kuna yeyote aliyewahi kubatizwa kwa kutumia "Katika jina la Baba, na la Mwana, na la Roho Mtakatifu."

MATHAYO 28:19
KUNUKULIWA AU KUTIIWA

Mimi ni mwanamume. Nina wazazi. Kwa hiyo mimi mwana. Siitwi mwana hilo si jina langu. Mwana ni jinsi nilivyo si mimi ni nani. Jina langu ni David. Pia mimi ni mume na Baba, Ingawaje kama nitaingia katika biashara kama vile kutia sahihi hundi au mkataba. Pande zinazohusika hazitajali jinsi nilivyo. Wanahitaji kujua mimi ni nani. Kama ninatia sahihi hundi mwana au Baba au mume, Banki haitakubali.

Hivyo vyeo si sawa na jina langu. Ninaweza kuwa na vyeo vingi, ila nguvu ipo katika jina langu. Baba mwana na Roho Mtakatifu si majina. Ni vyeo vinavyomueleza Mungu.

Baadhi wangeweza kusema kuwa kubatizwa kwa kusema Baba, mwana na Roho Mtakatifu ni sawa na kubatiza katika jina la Yesu. Mtu angeweza tu kumwomba mtu kama huyo kumtafadhalisha kutoa maandiko na hutapata kamwe. Kama kwa mantiki ya bishano kama hilo, ni udanganyifu tu.

Kumbuka kuwa Yesu alifunulia Mitume akili zao. Walitambua vizuri alimaanisha nini alipowaamuru kubatizwa katika JINA (umoja) la Baba, mwana na Roho Mtakatifu.

- **SWALI:** Jina la mwana ni nani?
- **JIBU:** Wakristo watasema, Yesu

- **SWALI**: Yesu alisema nini kuhusu jina la Baba?
- **JIBU:** "Mimi nimekuja kwa jina la Baba yangu..." (Yohana 5:43).

"Jina lako namewadhihirishia watu wale ulionipa..." (Yohana 17:6).

"Nami naliwajulisha jina lako (La Baba) tena nitawajulisha hilo..." (Yohana 17:26).

Biblia pia inasema, kuhusu jina la Yesu "amefanyika bora kupita malaika, kwa kadiri jina alilolirithi lilivyo tukufu kuliko lao" (Waebrania 1:4).

Kama nimekuambia kuwa nimerithi jina langu toka kwa baba yangu, na nimekuja kwa jina la baba yangu, usingekubali kutokana na hili jambo kuwa baba yangu na mimi tunatumika jina moja? Je mwana alilidhihirisha na kujulisha jina lingine lolote mbali na Yesu? Kutokana na hili ni lazima tujue kuwa jina la Baba ni Yesu. Kumbuka, Yesu alisema "Mimi na Baba yangu tu umoja" (Yohana 10:30).

- **SWALI:** Yesu alisema nini kuhusu Roho Mtakatifu?
- **JIBU:** "Lakini huyo msaidizi huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu..." (Yohana 14:26).

Tuseme nini basi kama jina la Roho Mtakatifu si Yesu?

Baada ya fahamu zao kufunuliwa na Yesu, Mitume waliendelea mbele wakatii amri si wakiirudia. Walitambua kuwa jina la Baba, mwana na Roho Mtakatifu ni Yesu na ndivyo walivyobatiza katika jina la Yesu. Tusingeweza kuokolewa kabisa kwa kunukuu tu amri za Bwana. Tunaokoka kwa hakika kama tutazitii.

Neno la Mungu linaonyesha kwa wazi kabisa kutokea siku ya Pentekoste mitume walitii amri ya Bwana, kwa kubatiza waongofu wao katika jina la Yesu. Huu ushahidi wa kimaandiko unajitosheleza wenyewe kutuongoza sisi katika kulitumia jina la Yesu kwenye maisha yetu.

Pia kuna jambo la historia la kufikiria wengine wataweka ushahidi wa kihistoria katika kiwango kile kile na maandiko. Tukumbuke hapa kuwa hakuna mamlaka ya juu zaidi ya neno la Mungu. Ingawaje tutatazama kumbukumbu za kihistoria kuona jinsi amri ya Bwana katika Mathayo 28:19 ilivyotumika.

Historia hutuambia kuwa kanisa la mwanzo lilianza kwa kubatiza katika jina la Yesu, lakini baadaye tendo hili lilibadilishwa na baadhi.

"Kila mahali katika vyanzo vya zamani kabisa imeelezwa kuwa" (Encyclopedia Britannica, vol.3, uk. 28).

"Kwa kujadili kuendelea kwa kanuni ya utatu huyu mwandishi anasema, Hii huonekana katika kanuni ya ubatizo ya Utatu ambayo ilichukua nafasi ya ubatizo wa mwanzo katika jina la Yesu kristo" (Historia ya kanisa la kikristo, Williston Walker).

"Kanuni ya ubatizo katika jina la Baba Mwana na Roho Mtakatifu ambayo inaonyeshwa kama ya kimapokeo na Justin Martyr, huenda isiwe ndiyo ya mwanzo kabisa ila ya mwanzo zaidi huenda ni kanuni fupi zaidi inayotumtaja Kristo" (Historia ya Dini ya Kikristo na Kanisa, Neander).

"Kanuni ya utatu (Mathayo 28:19) iliongezwa baadaye na wakristo wenye mawazo ya kupewa heshima" (Black's Bible Dictionary).

"Maelezo ya wazi ya ukimya wa Agano Jipya juu ya jina la utatu na kutumia kanuni nyingine katika matendo na Paulo ni kuwa hii kanuni nyingine ni ya mwanzo zaidi na kuwa kanuni ya Utatu ni tokeo la baadaye" (Ecnyclopedia of Region and Ethics, Hastings).

"Yesu ingawaje asingeweza kuwa amewapa wanafunzi wake huu utaratibu wa ubatizo (Mathayo 28:19), baada ya kufufuka kwake, kwa sababu Agano Jipya hutambua tu ubatizo mmoja katika jina la Yesu (Matendo 2:38; 8:16; 19:5; Wagalatia 3:27; Warumi 6:3; 1 Korintho 1:13-15), ambao bado unaendelea kutokea hata katika karne ya pili na ya tatu, wakati ambapo kanuni ya utatu inaonekana katika mathayo 28:19 na mara nyingine tena katika Didach 7:1 na Justini 1:61. Si jambo la kufikirika kuwa kanisa la Mitume halikutii amri iliyopigwa chapa ya Bwana ambayo hufikirika kuwa mamlaka ya juu kabisa" (The New Schaff Herzog Religions Encyclopedia).

Kwa wale wanaokubali maelezo kuwa mababa wa kanisa walishiriki moja kwa moja katika kubadilisha kanuni ya ubatizo, huu ugumu hautabakia, kwa kutaja kwa nafsi walijenga uthabiti wao juu ya Mathayo 28:19. Walakini kuna ushuhuda

wa kutosha kuwa andiko la Mathayo 28:19 kinatiliwa shaka na pia uwongo.

"(Mathayo 28:19) ni kipande cha katikati cha ushahidi wa maoni ya kimapokeo...kama ilikuwa si ya mashindano, hii ingekuwa ni ya uongo, ila uaminikaji wake umekanwa kwa misingi ya mashutumu ya kivitabu, upinzani wa kimaandishi, na Upinzani wa kihistoria" (Encyclopedia of Religion nad Ethics Hastings).

Kuhusu Mathayo 28:19 na maandishi mengine.

“Kwa kiwango chochote...tafsiri ya kitabu kinachopatikana katika namna ya kimapokeo...Ingawaje ni lazima ikumbukwe kuwa maandishi yaliyo bora zaidi yote ya Kiafrika kilatini cha kale na tafsiri ya kishamu cha kale vimeharibiwa kwa hivi sasa” (Encyclopedia of Region and Ethics, Hastings).

"Katika orodha pekee ambayo ingeweza kuonekana kuhifadhi maandishi ya kale yanayoitwa kisinai cha kishamu na maandishi ya kale kabisa ya kilatini...kurasa hazipo zinazoonyesha mwisho wa Mathayo" (F. C. Conybeare).

"Agizo la kubatiza katika jina la Utatu ni fundisho la baadaye lililopanuliwa. Baada ya maneno kuwabatiza katika jina la Baba na mwana, na Roho Mtakatifu. Labda tungesoma kwa urahisi ndani ya jina langu" (Dr. Peake, Peake's Bible Commentary).

Pengine muhutasari wa mfuatano ulioelezwa kwa akili za binadamu ulipotoa mpango wa mwanzo wa Mungu unaopatikana katika nukuu ifuatayo. "Mwanzo ibada inaonekana kutendeka katika jina la Kristo, lakini kabla mwisho wa karne ya kwanza kanuni ya utatu ilianza kutumika, kama ilivyothibitishwa katika Mathayo 28:19. Mara ya kwanza kuzamisha ilikuwa ni jambo la kawaida ila kadiri uamsho ulivyoenea katika nchi ambapo maji yaliyohitajika hayakupatikana ilionekana inatosha kumimina maji kisiwani au kunyunyiza kwa viganja. Katika siku za mwanzoni za umisionari (utume) waliotakiwa kubatizwa walikuwa waongofu watu wazima , lakini nguvu ya kiapo ilianza kuunganishwa na tendo ilianza kufanyika kwa manufaa ya watoto na hata kwa wafu" (Encyclopedia of Region:Vergilius Ferm).

Huu ni upotovu wa kutisha ambao tunaupata katika Neno la Mungu. Yote haya yanaleta swali lile lile alilouliza Petro siku ile ya Pentekoste.

TUTENDE JE?

Ni wazi kabisa kuwa hakuna siri ambayo makanisa mengi ya kikristo hayaoni ubatizo kama ni muhimu kwa wokovu. Si kusudi la huyu mwandishi kuthibitisha kanisa moja limekosea na lingine ni sahihi. Swali ambalo lingeulizwa ni hili: Ni nini vipimo vya kutumika katika kujua ni nini tu mpango wa wokovu.

Je, tunatakiwa kuchagua kujaribu ukweli? "Wakati wote unapokuwa mkweli katika kumwabudu Mungu wako, basi utaokoka."

Watu wanaounga mkono wazo hili wanasema kwa hakika kuwa fundisho si muhimu. Ingawaje, Biblia inakataa.

"Nao waniabudu bure, wakifundisha mafundisho yaliyo maagizo ya wanadamu" (Marko 7:7).

Shetani alimshawishi Hawa usijali, kuwa Mungu alisema nini. "Endelea tu fanya unavyopenda." Kaini na wengineo wamegundua kwa masikitiko yao kuwa Mungu hakubali wale wenye mfano wa utauwa, ila wakikana nguvu zake. Natumaini kuwa mpaka sasa tutakuwa tumeshathibitisha kuwa kuna nguvu kuu katika jina la Yesu. Haijalishi inajaribu kiasi gani, hatuwezi kukubali "Uamini rahisi" ulio mashuhuri leo badala ya uti kwa Neno la Mungu.

Lazima tuufuate mpango wa Mungu kama tunataka kuokolewa. Hakuna njia nyingine itakayofanikiwa, haijalishi tunaitumia kwa utiifu namna gani.

"Si kila mtu aniabiaye, Bwana, Bwana, atakayeingia katika Ufalme wa mbinguni, bali ni yeye afanyaye mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni" (Mathayo 7:21).

Kwa dhahiri hakuna upungufu wa kimaandiko kuhusu wokovu. Ndicho kiini cha Biblia. Kinachofuata ni kuchukua maelezo mengi yahusuyo wokovu yaliyomo katika Neno la Mungu.

Biblia inasema tunaokolewa kwa-:

- Unyenyekevu (Ayubu 22:9)
- Rehema (Zaburi 109:26)
- Neno la Mungu (Yakobo 1:22)
- Ubatizo (1 Petro 3:21)
- Imani (Luka 7:50)
- Ukiri / Maungamo (Warumi 10:9)
- Kuzaliwa mara ya pili (Yohana 3:5:)
- Toba (2 Wakorintho 7:10)
- Injili (1 Wakorintho 15:1-21)
- Roho iliyovunjika (Zaburi 34:18)
- Uvumilivu kwa Mungu (2 Petro3:15)
- Kumjua Mungu (Yohana 17:3)
- Kuwa mnyofu katika moyo (Zaburi 7:10)
- Kuliitia jina la Bwana (Warumi 13:13; Matendo 2:21)
- Unyenyekevu (Zaburi 76:9)
- Mahubiri (1 Wakorintho 1:21)
- Kuamini (Yohana 3:16)
- Wavumilivu (Mathayo 10:22)
- Jina (Matendo 4:12)
- Tumaini (Warumi 8:24)
- Neema (Waefeso 2:5)
- Nguvu ya Mungu (1 Petro 1:5)

Kwa kuongeza orodha ya mifano ya maandiko yaliyotolewa hapo juu, yapo mawazo kama, "Mpokee Bwana kama mwokozi wako," Ambapo hakuna kigezo chochote cha kimaandiko. Hapa tutahusikia tu na vigezo vya kimaandiko.

Kwa dhahiri hakuna upungufu wa maandiko ya kurejea juu ya somo hili. Ni dhahiri kabisa kuwa Biblia hutoa matamko tofauti kuhusu wokovu wetu. Inakuwaje basi tunaamua tamko lipi la wokovu ni muhimu na yapi ni maoni au "Tunaikiza keki kwa sukari?"

Hakuna mwongozo wa kibiblia kutenga tamko moja la wokovu kama muhimu au la kuliko lingine.

Ili kuwa na "Utakatifu ambao bila kuwa nao hapana mtu atakamwona

Bwana," Lazima nimfananie sura yake katika mambo mengi. Mwishowe lazima nimpendeze Mungu kwa masharti yake, na Yeye atakuwa hakimu. Huu utakuwa mwelekeo wa maisha yangu, kukua katika neema, na kufananishwa na sura Yake zaidi na zaidi. Katika hili Bwana aliahidi kuwa Roho Mtakatifu atatuongoza katika kweli yote.

Kama Paulo, sijihesabu kuwa nimefika, ila naukaza mwendo. Inawezekana mpango kamili wa Mungu kwa wokovu wetu ulielezwa kule mwanzo Mungu aliposema, "Natufanye mtu kwa sura yetu." Mwishowe huu ndiyo mwisho wa waliookoka; "Tutafanana na Yeye, kwa maana tutamwona kama alivyo...." Kwa sasa, kwa kuwa sote tunaona kama kupitia kioo cheusi, baadhi labda watakuwa karibu zaidi na Sura ya Kristo kuliko wengine. Ingawaje, jinsi mtu anapofanyika mwana wa Mungu lazima iwe ni ile ile na mwingine. Ujumbe huu, unaodumu kama kigawo kidogo cha shirika kwa jamii yote ya wakristo, ni Injili rahisi ya Ufalme.

INJILI YA UFALME

Ufalme umetajwa mara 144 katika Agano Jipya, sehemu kadhaa unaitwa Ufalme wa mbinguni, Ufalme wa Mungu na kadhalika. kuzaliwa kwa Yesu kulitangaza kuja kwa Ufalme.

"Ataimiliki nyumba ya Yakobo hata milele, na Ufalme wake utakuwa hauna mwisho" (Luka 1:33).

Huu haukuwa tu ni Ufalme wa Duniani. Ufalme wa Yesu Kristo ni wa milele na wa mbinguni.

"Maana hivi mtaruzukiwa kwa ukarimu kuingia katika Ufalme wa milele wa Bwana wetu, mwokozi wetu Yesu Kristo" (2 Petro 1:11).

Tutapata zaidi katika mifano na mafundisho ya Yesu kuhusu Ufalme. Mengi ya haya hayakuweza kufahamika vizuri kwa wanafunzi lakini ilfanyika kitovu cha mafundisho yao na mahubiri.

"Lakini walipomwamini Filipo akihubiri habari njema za ufalme wa Mungu na jina lake Yesu Kristo, wakabatizwa, wanaume na wanawake" (Matendo 8:12).

Jambo hili la kuona kutambua na kufanya yatakiwayo kwa kuingia katika Ufalme wa Mungu yanapatikana katika mafundisho ya Yesu kwa Nikodemo.

"Yesu akajibu akamwambia, Amin amin nakuambia. mtu asipozaliwa mara ya pili hawezi kuuona ufalme wa Mungu, Nikoemo akamwambia, awezaje mtu kuzaliwa mara piliakiwa mzee? aweza kuingia tumboni mwa mamaye ten mara ya pili akazaliwa? Yesu akajibu akamwambia, Amin amin nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho hawezi kuingigia katika ufalme wa Mungu" (Yohana 3:3-5).

Hitaji la kuzaliwa mara ya pili limetolewa hapa na kiingilio katika ufalme. Mengi yametolewa kwa kuzaliwa mara ya pili katika mzunguko wa Ukristo leo.
Inaonekana hawakuweza kuutambua ufalme wa Mungu mpaka walipouingia Hata hivyo, kuhusu kuzaliwa mara ya pili katika mizunguko ya Ukristo hivi leo. Ingawaje, huonekana kuwa mara nyingi suala la kuzaliwa kwa maji na kwa Roho limesahaulika. Yesu alieleza kuwa alikuwa akifafanua uzao wa Kiroho. Kuzaliwa kwa maji anazungumzia dhahiri kuhusu ubatizo. Kuzaliwa kwa Roho kulionyeshwa kabla kama kivuli Yesu alipowaambia wanafunzi wake," Nipo pamoja nanyi sasa, ila nitakuwa ndani yenu." Hili lilitimizwa katika siku ya Pentekoste.

Ilikuwa ni tabia ya Yesu kufundisha kanuni (Mifano) kuliko vitu halisi Hivyo

tunaona kuwa Yesu hakuelezea kikamilifu suala la kuuingia katika Ufalme, ila badala yake aliitegamea huduma ya wanafunzi wake.

"Nami nitakupa wewe funguo za Ufalme wa mbinguni na lolote utakalolifunga duniani, litakuwa limefungwa mbinguni: na lolote utakalolifungua duniani litakuwa limefunguliwa mbinguni" (Mathayo 16:19).

Yesu alimchunguza Petro kwa kufahamu kwake kuwa Yesu ni nani, ulikuwa ni Ufunuo aliopewa na Baba na huo ungekuwa ni mwamba ambao juu yake kanisa lingejengwa. Baadhi waliamini kimakosa kuwa Petro alikuwa ndiye Mwamba. Neno hapa linaeleza kuwa ufunuo wa Yesu Kristo ni jiwe la Msingi wa kanisa. Ndipo Petro alipojulishwa kuwa angetumiwa kufungua mlango wa kwenye Ufalme wa mbinguni. Kama vile kazi ya funguo ni kufunga na kufungua, hivyo aliambiwa kuwa angekuwa na nguvu za kufunga na kufungua. Matumizi ya funguo yalianza siku ile ya Pentekoste.

Bila shaka inaonekana baadhi ya wanafunzi hawakuonekana kutambua kwa hakika maana ya Ufalme hata baada ya kufufuka kwa Yesu.

"Wale aliowadhihirishia nafsi yake, kwa dalili nyingi, baada ya kuteswa kwake, ya kwamba yu hai akiwatokea muda wa siku arobaini, na kuyanena mambo yaliyohusu Ufalme wa Mungu" (Matendo 1:3).

"Basi walipokutanika, wakamwuliza, wakisema, Je! Bwana, wakati huu ndipo unapowarudishia Israeli Ufalme? Akawaambia, si kazi yenu kujua nyakati wala majira, Baba alivyoyaweka katika mamlaka yake mwenyewe. Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu:nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Matendo 1:6-8).

Jibu Yesu alilotoa kuhusu udadisi wao kuhusu Ufalme huonyesha pasipo kosa muunganiko kati ya Ufalme wa Mungu na Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Pia tazama maneno ya Paulo kuhusu jambo hili. "Maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu" (Warumi 14:17).

Wakati ahadi ya Roho mtakatifu ilipowashukia, mara tunamwona Petro anahubiri ujumbe wa kwanza wa kanisa la Agano Jipya. Wakati makutano walipopaza sauti kwa ushawishi, "Tufanye nini?" Petro akafungua mlango wa kwenye Ufalme wa mbinguni kwa maneno haya:

"Petro akawaambia, Tubuni makabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu na kwa watoto wenu, na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie" (Matendo 2:38-39).

Siyo kwa bahati njema kuwa amri ya Petro kubatizwa na kujazwa na Roho ili kutimizwa vyema azimio la Yesu kuhusu kuzaliwa Upya. Ubatizo katika jina liokoalo la Yesu na Ubatizo utoao uzima wa Roho mlango uliofunguliwa wa uzima wa milele. Tunazaliwa kwa maji, na kwa kumpokea Roho Mtakatifu tunazaliwa kwa Roho. Lazima tujue kuwa wakati Petro alipotumiwa na Mungu kufungua Mlango wa wokovu kwa mataifa katika matendo 10, alitumia kanuni ileile kama ya mlango wa pili wa Matendo.

"...Ndipo Petro akajibu ni nani awezaye kukataza naji, hawa wasibatizwe, watu waliompokea Roho Mtakatifu vile vile kama sisi? Akaamuru wabatizwe kwa jina lake Yesu Kristo" (Matendo 10:46-48).

Hatudharau ile sehemu ihusuyo toba. Hii ni mauti iliyozungumziwa katika

Warumi mlango wa sita. Haiwezekani kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu pasipo toba kwanza.

Biblia inatuambia kuwa mtu yeyote asiye na Roho wa Kristo, huyo siyo wake (Warumi 8:9). Kuitwa mtoto halisi, mtu lazima azaliwe (apewe uhai) na mimi, na pia achukue jina langu. Je hili halitimizwi kwa kutii Matendo 2:38? Kwa ubatizo tunachukua jina la Yesu na tumezaliwa kwa maji. Kwa kumpokea Roho Mtakatifu tunazaliwa kwa Roho. Hii ndiyo Injili ya Ufalme ambayo Mitume waliihubiri.

"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walilopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12).

NYONGEZA

"Kuhusu uzamisho wa Utatu: Hivi kwa uwazi kabisa ni vya kivitendo na viligunduliwa kuelezea desturi iliyopo, ambayo kanisa imechukua toka njia zake za kipagani, kwa sababu utakaso wa kipagani ulikuwa kwa kawaida ni wa utatu" (Encyclopedia Britannica, 11th Edition, Vol. 3).

"Namna ya mwanzoni kabisa ya mababu iliyotumika ilikuwa pasipo shaka yoyote ni kuzamisha" (Catholic Encyclopedia, Vol. 2, p. 261).

"Katika kusoma kwangu nimeweza kuthibitisha haya mashaka ya usahihi wa kitabu cha Mathayo 28:19 kwa kutumia ushahidi wa waalimu wa kale dhidi yake, Kwa uzito kabisa kuwa hapo baadaye suala lisilobadilika kabisa la miungu litasinyaa kwa kupachika juu yake kanuni iliyoundwa kabisa, Wakati ambapo walioangaziwa zaidi watalikataa moja kwa moja kama walivyofanya kitabu chenzake cha 'Mashahidi wa tatu'" (F. C. Conybeare).

"Ushahidi wa muda mrefu wa hii mistari mitatu ya upinzani (upinzani wa kivitabu, Upinzani halisi, upinzani wa kihistoria) ni kuwa kinyume kabisa kuona kuwa Mathayo 28:19 (katika AV) inawakisisha maneno halisi ya Kristo" (Encyclopedia of Region and Ethics, Hastings).

Katika tafsiri yake halisi ya Biblia, Young ameweka jina la Utatu katika Mathayo 28:19 katika mabano, hii inaonyesha maneno haya yanashukiwa uhalisi wake (Dr. Robert Young).

Professor Harnack anaondoa kitabu cha (Mathayo 28:19) akiyapuuza kabisa kuwa "Si neno la Bwana" (Professor Harnack, History of Dogma).

Namna ya mwanzoni ya maneno yalikuwa ni katika jina lake Yesu Kristo au Bwana Yesu, Ubatizo katika utatu ulikuja baadaye. (Dictionary of the Bible, Scribners).

Kanisa la kwanza wakati wote walibatiza katika jina la Bwana Yesu mpaka Utatu ulipoanzishwa, baada ya hapo walibatizwa katika jina la Baba, mwana na Roho Mtakatifu (Encylopedia ya Canney).

ROHO WA AHADI

"Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina Roho yangu juu ya wote wenye mwili: na wana wenu, waume kwa wake, watatabiri, wazee wenu

wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono: tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake, katika siku zile nitamimina roho yangu" (Yoeli 2:28-29).

Ubatizo wa Roho Mtakatifu uliahidiwa kale kwa watu wa aina zote. Baada ya mamia ya miaka ambayo kutembea kwa Roho wa Mungu kulionekana kutokea kwa manabii wachache tu, Hii ilikuwa ni ahadi ya kushangaza kabisa. Yesu alirejea unabii wa Yoeli kuhusu kumwagwa kwa Roho Mtakatifu alipowafariji wanafunzi wake kuhusu kuondoka kwake kulikokaribia sana.

"Nami nitamwomba Baba, naye atawapa Msaidizi mwingine, ili akae nanyi hata milele: Ndiye Roho wa kweli ambaye ulimwengu hauwezi kumpokea, kwa kuwa haumwoni wala haumtambui: bali ninyi mnamtambua, maana anakaa kwenu naye atakuwa ndani yenu" (Yohana 14:16-17).

Kabla tu ya kupaa kwake Yesu aliwapa wanafunzi wake maelekezo kuhusu ni kwa namna gani wangempokea Roho Mtakatifu.

"Natazama, nawaletea juu yenu ahadi ya Baba yangu: lakini kaeni humu mjini hata mvikwe uweza utokao juu" (Luka 24:49).

Walitambua kutokana na tamko la Yesu lililopita kuwa Alikuwa anaongea kuhusu nguvu ya Roho Mtakatifu.

"Lakini mtapokea nguvu akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu..." (Matendo 1:8).

Baada ya kupaa walirudi Yerusalemu kwa furaha kubwa na wakaendelea katika hekalu, wakimsifu na kumwabudu Mungu. Hivyo wakatii maelekezo yake, wakisubiri kumiminwa kwa Roho kulikotokea siku ya Pentekoste.

"Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote pamoja. Kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukienda kasi, ukaijaza nyumba yote waliyokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka" (Matendo 2:1-4).

Huu utimilifu wa ajabu wa ahadi ya Mungu ulisikika mbali, ukivuta mkutano wa maelfu kutoka katika kila taifa chini ya mbingu. Hawakuelezewa tabia ya ajabu ya wanafunzi. Walilolisikia ilikuwa ni wanafunzi 120 wakinena sifa za Mungu katika lugha zao tofauti. Baadhi wakadhihaki wakisema walikuwa wamelewa. Ila Petro akasema akatoa maelezo moja kwa moja kitu kilichoashiria mwanzo wa kanisa la Agano Jipya.

"Sivyo mnavyodhani; watu hawakuelewa kwa maana ni saa tatu ya mchana; lakini jambo hili ni lilelililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli. Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu na wana wenu na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto" (Matendo 2:15-17).

Huu utimiaji wa ahadi ya Mungu ilianzisha kitu ambacho kimeendelea mpaka siku hii ya leo kuwa nguvu itoayo uzima wa Kanisa la Agano Jipya. Yapo mambo mengi kwa hii nguvu ambayo ambayo Mungu ametupa sisi. Katika yafuatayo tunatamani kutazama kipawa hiki cha ajabu.

WOKOVU

"Yesu akajibu, Amin amini nakuambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni roho" (Yohana 3:5-6).

"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu, Kwa kuwa ahadi hii ni ajili yenu,na watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie" (Matendo 2:38-39).

Kutokana na maneno ya Yesu tunajifunza kuwa ni lazima tuzaliwe kwa Roho ili tuweze kuingia katika Ufalme. Kutokana na maneno ya mitume Petro tunajifunza jinsi ya kuzaliwa mara ya pili.

NGUVU YA UFUFUO

"Lakini ikiwa Roho wake yeye aliyemfufua Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu ataihusisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu" (Warumi 8:11).

Pasipo nguvu ya Roho, tumaini letu la Ufufuo litakuwa wapi? Msisitizo hapa unawekwa juu ya hakika ya kuwa Roho ni lazima akae ndani yetu. Andiko linasema, "Kristo ndani yenu, tumaini la utukufu" (Wakolosai 1:27).

WATOTO WA MUNGU

"Lakini ikiwa Roho wa Mungu anakaa ndani yenu, ninyi hamwufuatii mwili, lakini mtu awaye yote asipokuwa na Roho wa Kristo, huyo si wake" (Warumi 8:9).

Kupokelewa kama mtoto wa Mungu, maandiko yanatufundisha kuwa ni lazima tuwe na Roho wa Mungu anayekaa ndani yetu sisi.

“Kwa kuwa wote wanaongozwa na Roho wa Mungu, hao ndio wana wa Mungu kwa kuwa hamkupokea tena roho ya utumwa iletayo hofu; bali mlipokea roho ya kufanywa wana ambayo kwa hiyo twalia, Aba, yaani baba roho mwenyewe hushuhudia pamoja na roho zetu, ya kuwa sisi tu watoto wa Mungu" (Warumi 8:14-16).

MWENENDO WA KIKRISTO

“Basi nasema, enendeni kwa Roho, wala hamtazilimiza kamwe tamaa za mwili" (Wagalatia 5:16).

"Sasa basi hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu" (Warumi 8:1).

"Kwa maana kama mkiishi kwa kufuata mambo ya mwili, mwataka kufa; Bali kama mkiyafisha matendo ya mwili kwa Roho, mtaishi" (Warumi 8:13).

Katika mwanga wa maandiko hapo juu, inaonekana kuwa haiwezekani kuishi maisha yanayompendeza Mungu kwa hakika pasipo nguvu na mwelekeo wa Roho.

NGUVU ZA ROHO

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu..." (Matendo 1:8).

"Na neno langu ni kuhubiri kwangu hakukuwa kwa maneno ya hekima yenye kushawishi akili za watu, bali kwa dalili za Roho na za nguvu" (1 Wakorintho 2:4).

UFUNUO WA KWELI

"Lakini yeye atakapokuja, huyo Roho wa kweli, atawaongoza awatie kwenye kweli yote..." (Yohana 16:13).

"Lakini kama ilivyoandikwa, mambo ambayo jicho halikuyaona wala sikio halikuyasikia, (wala hayakuingia katika moyo wa mwanadamu) mambo ambayo Mungu aliwaandalia wampendao. Lakini Mungu ametufunulia sisi kwa Roho maana Roho huchunguza yote, hata mafumbo ya Mungu" (1 Wakorintho 2:9-10).

Kwa ufahamu wa mwilini wenyewe hauwezi kuelewa sheria rahisi kabisa za Ufalme wa Mungu. Kama Yesu alivyomwambia Petro, nyama na damu havikumfunulia ile kweli. Mawazo ya kiroho yanafahamika tu kwa Ufunuo utolewao na Roho. Wanafunzi waliitwa wajinga na wasioelimika, lakini walipewa kujua siri za Kiroho. Mtume Paulo msomi aliongoka kutokana na mapokeo na kuipata kweli Swali lake lilipojibiwa kwa maneno matatu; "Mimi ni Yesu"

"Wakati ule Yesu akajibu, akasema, Na kushukuru, Baba, Bwana wa Mbingu na nchi kwa kuwa mambo haya uliwaficha wenye hekima na akili, ukawafunulia watoto wachanga" (Mathayo 11:25).

ROHO WA MOYO WA KIASI

"Maana Mungu hakutupa roho ya woga, bali ya nguvu na ya upendo na ya moyo wa kiasi" (2 Timotheo 1:7)

Mara nyingi mvurugiko wa akili unasababishwa na masumbufu ya mazingira yetu. Woga ni mwandani wa kawaida wa wengi hivi leo. Kwa kweli, Biblia inasema kuwa siku za mwisho mioyo ya wengi itazimia kwa sababu ya woga. Chini ya nguvu za roho za Ulimwengu huu, watu hufanya mambo mengi ya ajabu na ya kutisha. Roho wa Mungu ni Silaha yetu kinyume cha kazi ya Uharibifu ya roho ya Shetani.

KARAMA ZA ROHO

“Maana mtu mmoja kwa Roho apewa neno la hekima na mwingine neno la maarifa apendavyo Roho yeye yule; Mwingine Imani katika Roho yeye yule na mwingine karama za kuponya katika Roho yule, na mwingine matendo ya miujiza na mwingine unabii na mwingine kupambanua roho; mwingine aina za ligha; na mwingine tafsiri za lugha: Lakini kazi zote huzitenda Roho huyo mmoja, yeye yule, akimgawia kila mtu peke yake kama apendavyo yeye" (1 Wakorintho 12:8-11).

Hizi karama zimetolewa kwa Kanisa na Mungu kwa njia ya huduma ya Roho wake. Karama hazitoki sehemu nyingine yeyote ila tu ni kazi ya Roho wa Mungu

katika maisha yetu. Kwa kweli haingewezekana kupata moja au zaidi ya karama hizi za Roho kutenda kazi katika maisha yetu pasipo kwanza kumpokea Roho Mtakatifu.

Karama tisa zilizoorodheshwa katika 1 Wakorintho 12 zinatokea katika makundi matatu au aina za karama. Hizi ni karama za ujuzi, karama za nguvu na za unabii au karama za kuzungumza.

Karama za ufahamu zinatolewa kwetu kutufunulia kwa njia ya Roho mambo ambayo vinginevyo tusingevijua. Hizi ni karama za Neno la Hekima, Neno la maarifa na kupambanua roho lazima ifahamike kuwa hakuna karama kati ya hizi zinazoleta ujuzi wa mambo yote au kutokukosea. Ni msaada tunaopewa sisi wakati kwa wakati na si mtiririko usiokoma wa maelekezo toka juu.

Karama za nguvu ni zinatolewa maana maalumu kwa kusudi la kuhudumu. Hizi ni Imani, karama za uponyaji na kutenda miujiza. Hizi karama mara nyingi zinaleta matokeo ya ajabu na Usikivu zaidi. Ni muhimu kuwa wakati wote tukumbuke chanzo cha nguvu na mwelekeo ambao sifa zinahitajika kupelekwa. Kutumia nguvu za Mungu kwa Utukufu wetu wenyewe ni kudhalilisha karama za Roho.

Karama za kutamka kinabii ni za upako maalumu wa Roho hizi ni unabii, aina za lugha na tafsiri ya lugha. Karama hizi kwa kawaida zimeeleweka vibaya na zinatakiwa kupambanuliwa kutokana na Neno la Mungu. Hakuna ujumbe unaotoka kwa Mungu utakaopinga Neno lake. Lazima ikumbukwe kuwa vipo vyanzo vitatu vya uvuvio; Roho wa Mungu, roho zetu wenyewe za binadamu na roho wa shetani. Haya matamshi maalumu yanapotolewa, inabidi tuzijaribu roho, kama zinatokana na Mungu. Kufanya kosa la mioyo yetu wenyewe kuwa ni sauti ya Mungu siyo dhambi ni kosa ambalo tunahitaji kumwomba Mungu atusaidie kulishinda. Kwa maana karama hizi ni rahisi kizitumia vibaya, Uongozi wa hekima pamoja na kupambanua roho vitatoa masahihisho kama inavyotakiwa. Hatari kubwa wanapokosa upambanuzi wa kiroho na ujasiri na hekima kutoa masahihisho. Hatimaye karama hizi huja chini ya mamlaka ya huduma. Pia lazima ijulikane kuwa roho wa manabii wale wanaosema kuwa hawawezi kuzuia tamshi lililotiwa upako wanakosea kwa uhakika wapo katika kutawala kwa sababu lile tamshi halitoki kwa Mungu ila hutoka mioyoni mwao wenyewe. Wote waliobarikiwa na aina hii ya karama lazima watambue na kutii mamlaka ambayo Mungu ameiweka katika Uongozi wa kanisa. Pia kunena lugha ambako kunafuatana kwanza na kujazwa Roho Mtakatifu kusichanganywe na karama za Roho, kwa hakika kabla ya kupokea karama za Rohoni ni muhimu kwanza kupokea Roho.

Maoni haya juu ya karama za Roho zimemaanishwa tu kwa kutoa ufahamu wa jumla juu ya karama. Kila karama ya Roho ni pekee yenywe na namna ya utendaji inaweza kutofautiana kutoka mtu hadi mtu. Biblia inatamka kuwa karama zinatakiwa zitafutwe kwa manufaa yetu ya kiroho.

UHURU WA ROHO

"Basi Bwana ndiye Roho: Walakini alipo Roho wa Bwana, hapo ndipo penye uhuru" (2 Wakorintho 3:17).

Ningeweza kuongezea kutokana na uzoefu wangu mwenyewe katika

kuhudumu kuwa alipo roho wa Shetani, pana kizuizi kwa kitu chochote kimtukuzacho Bwana au chenye kuwabariki watu. Hata hivyo, Pia tunajua kuwa kama una Roho wa Mungu ndani yako, basi "Aliye ndani yenu ni mkuu kuliko aliye ulimwenguni."

MUHURI WA ROHO

"Nanyi pia katika huyo mmekwisha kulisikia neno la kweli, habari njema za wokovu wenu: tena mmekwisha kumwamini na kutiwa muhuri na Roho yule wa ahadi aliye mtakatifu. Ndiye aliyekaribuni ya urithi wetu, ili kuleta ukombozi wa milki yake, kuwa sifa ya Utukufu wake" (Waefeso 1:13-14).

KUOMBA KATIKA ROHO MTAKATIFU

"Kwa sala zote na maombi mkisali kila wakati katika Roho..." (Waefeso 6:18).

"Imekuwaje, basi? Nitaomba kwa roho, tena nitaomba kwa akili pia..." (1 Wakorintho 14:15).

"Kadhalika Roho naye hutusaidia udhaifu wetu, kwa maana hatujui kuomba itupasavyo: lakini Roho mwenyewe hutuombea kwa kuugua kusikoweza kutamkwa" (Warumi 8:26).

Mara unapoomba katika Roho umepata njia yenye nguvu ya kuendea baraka. Maombi na Imani ni rasilimali isiyo na mashaka yenye nguvu kuu tuliyonayo.

KUVUTWA NA ROHO

"Na Roho na Bibi arusi wasema, njoo! Naye mwenye kiu na aje: na yeye atakaye na ayatwae maji ya uzima bure" (Ufunuo 22:17).

"Hakuna mtu awezaye kuja kwangu, asipovutwa na Baba aliyenipokea..." (Yohana 6:44).

"Nami nikiinuliwa juu ya nchi, nitawavuta wote kwangu" (Yohana 12:32).

Kuhubiri au kushuhudia pasipo upako wa Roho Mtakatifu ni tendo lisilo na maana Roho Mtakatifu ndiye muhubiri halisi, Sisi ni vipaza sauti tu. Kama unataka kuwa mvuna mioyo, kwanza pa upako.

ULINZI KATIKA ROHO

"...Maana yeye atakuja kama mkondo wa mto ufurikao, uendeshwao kwa pumzi ya Bwana" (Isaya 59:19).

TUNDA LA ROHO

"Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilifu, utu wema, fadhili uaminifu upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria" (Wagalatia 5:22-23).

Inawezekana katika muda mrefu jaribu la mwisho kwa mtu aliyejazwa Roho ni kuzaa ni kuzaa tunda la Roho. Hili siyo ajabu kama kufufua wafu, au kuhubiri katika upako lakini ni muhimu hakika kwa Mungu. Sifa zilizoorodheshwa chini ya Tunda la Roho ni sifa za Mungu. Hatima ya kazi ya Roho Mtakatifu ni kutufanya sisi

katika sura ya Mungu wetu. Tungetakiwa zaidi tutoe neno la hekima au kutumia karama ya Imani,kuliko kuonyesha uvumilivu, ila Mungu wetu anatazamia tunda yule aliye ulaani mtini kwa sababu ya kukosa kwake kazi ya Roho yupo pale. Msitari wa 25 wa Wagalatia mlango wa 5 unatuambia, "Kama mkiishi katika Roho, tuenende katika Roho."

Yote haya husaidia kutuonyesha sisi umuhimu kamili wa kwetu sisi kujazwa na Roho wako watu wengi wanaojitahidi kumpendeza Mungu, na mara nyingi nguvu ya Roho Mtakatifu ni dhahiri katika maisha yao. Hata hivyo, pasipo kujazwa na Roho Mtkatifu hatuwezi kutumaini kufikia utimilifu wa kiroho wa mpango wa Mungu kwa ajili yetu. Petro alikuwa ni mmoja wapo wa mfano huu mzuri wa kweli.

Ingawaje Mungu alikuwa pamoja naye mtu wa mwili asiyejua chochote mpaka ujazo wa Roho Mtakatifu uliompa nguvu na mwelekeo aliohitaji. Inahuzunisha kuona wale wanaodai kuwa wamepokea Roho Mtakatifu ila kwa kweli hawajajazwa Roho. Mtu anaweza kuwa mwema anayejitoa dhabihu na kumpenda Mungu kwa dhati, ila pasipo kujazwa Roho Mtakatifu anakosa nguvu anayoihitaji. Kwa kweli si kwa nguvu wala kwa uweza, ila kwa Roho wa Bwana ndipo tunapata ushindi juu ya dhambi, Shetani na mwili kwa kuwa na haya ya kutosha, Bwana hajatuacha gizani kuhusu kujazwa na Roho Mtakatifu. Ametupa ishara ya kwanza ya kujazwa na Roho Mtakatifu,

"Na wale waliotahiriwa, walioamini wakashangaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha, na kumwadhimisha Mungu..." (Matendo 10:45-46).

Huu Ushahidi wa kunena kwa lugha unabaki leo kama kithibitisho cha mwanzo cha kujazwa na Roho Mtakatifu. Kinachofuatia na unenaji wa kweli hii ya Biblia, inayoitwa na wengine kama fundisho la ushahidi.

FUNDISHO LA USHAHIDI

Tunaanza kwa kutoa maana ya Fundisho la Ushahidi.

Fundisho la Ushahidi ni fundisho kuwa kuna ishara wazi au Ushahidi ambao unafuatana na kujazwa Roho Mtakatifu. Huu shahidi wa kwanza unaonyesha kuwa mtu amepata batizo wa Roho Mtakatifu ni kunena kwa lugha. Wakati ishara nyingine zitafuatilia, kama vile tunda la Roho n.k., ushahidi wa kunena kwa lugha ni ishara ya mwanzo ya ubatizo katika Roho.

Hili fundisho husema kuwa kunena kwa lugha wakati wote hufuatilia kujazwa na Roho Mtakatifu. Halisemi kuwa hakuna mtembeo wa Roho wa Mungu pasipo kunena kwa lugha.Kutoa tamko kama hilo ingekuwa si kimaandiko pia kutokuwa sahihi kutokana na matukio ya wengi. Kwa hakika wote tulivutwa na Roho wa Mungu kutubu dhambi zetu. Kornelio, Sauli wa Tarso na waongofu wa Samaria wote hawa ni mfano wa watu ambao waliongozwa na Roho wa Mungu kabla ya Ubatizo wao katika Roho Mtakatifu.

Hata hivyo, kuna mpaka ambao ni kwa kiwango gani mtu anaweza kuendelea kiroho pasipo kujazwa Roho. Ushawishi wa Roho katika kujazwa

kunaweza kufananishwa na utendaji wa uhai uliko tumboni. ni kweli kuna uhai hakika. Ingawaje, kuna tofauti kubwa kati ya utungwaji wa mimba na kuzaa.

Kuzaliwa kwa Roho ni kupata Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Kama vile mtoto aliyezaliwa hulia mara baada ya kuzaliwa tunalia Abba, Baba na Roho akishuhudia na Roho zetu kuwa tu watoto wa Mungu. Ukuaji unaoendelea na mabadiliko vile vile na wokovu ni vitu muhimu kuzaliwa kwa kweli kiroho. Karama za Roho wa Mungu katika maisha yetu, ni maendeleo ambayo hufuatia kuzaliwa kwa Roho.

Pengine itasaidia kuleta suala la kunena kwa lugha ili kulitazama kama tungetambua kwa nini Mungu alichagua kunena kwa lugha kama ishara. Katika Neno la Mungu tunajifunza kuwa ulimi ni kiungo kiovu sana.

"...Mtu asiyejikwaa katika kunena, huyo ni mtu mkamilifu, awezaye kuuzuia na mwili wake wote kama kwa lijamu. Bali ulimi hakuna awezaye kuufuga: ni uovu usiotulia, umejaa sumu iletayo mauti" (Yakobo 3:2, 8).

Kuna yeyote ulimwenguni wote asiyeweza kusema amen kwa maandiko hayo hapo juu? Ninaweza nikachukia na kujaribiwa kupiga kwa ngumi yangu, ila mkono wangu unazuiwa. wengi wetu hatujapewa kupiga teke, ngumi, kichwa na kadhalika. Haya ni matendo tuliyojifunza kuyatawala. Wangapi wetu wanaweza kusema tunaweza kutawala sawa sawa ndimi zetu? Mungu aliyetuumba sisi anatambua ulimwengu wa uovu ule ulio katika ndimi zetu. Kwa sababu hiyo, Aliamua sisi tumpe autawale Yeye, ili tuonyeshe pamoja na Mungu kuwa Yeye hakika ni Bwana wa utu wetu wote. Kunena kwa lugha ni suala la kushiriki na Roho wa Mungu kwa hakika hatuwezi kutenda huu muujiza sisi wenyewe, na Mungu hatatufanya tunene kwa lugha bila ridhaa na ushirikiano wetu. Hivyo kunena kwa lugha ni Ushahidi kuwa tumeyatoa kabisa kabisa mapenzi yetu kwa Mungu, na pia ni Bwana halisi katika maisha yetu.

Hakuna kujifunza kwa hili somo kungeweza kukamilika pasipo kutazama kutoka maandiko namna ambayo Roho Mtakatifu alitolewa.

Kwanza kabisa tunaona kutokana na Unabii wa Yoeli kuwa kumwagwa kwa Roho wa Mungu kulikuwa kwa watu wa namna zote.

"Hata itakuwa, baada ya hayo, ya kwamba nitamimina roho yangu juu ya wote wenye mwili: na wana wenu, wanaume kwa wake, watatabiri, wazee wenu wataota ndoto, na vijana wenu wataona maono: tena juu ya watumishi wenu, wanaume kwa wanawake katika siku zile, nitamimina roho yangu" (Yoeli 2:28-29).

Kusoma unabii huu pamoja na tangazo la Petro siku ile ya Pentekoste hutuhakikishia kuwa Mungu hutoa karama hii kwa kila kiwango cha jamii na kila Umri.

"Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe mmoja kwa jina lake Yesu kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu na kwa watu wote walio mbali na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie" (Matendo 2:38-39).

Wale watakaopinga kuwa kujazwa na Roho Mtakatifu kimiujiza kulikuwa ni kwa mitume tu au kwa kanisa la kwanza hawana msingi wa kimaandiko. Kwa kweli hakuna maelezo ya kimaandiko katika hali katika yoyote linatoa mpaka wa kumwagwa kwa Roho Mtakatifu. Ametolewa kwa yeyote anaye tamani kumpokea na anayetimiza mambo muhimu ya toba na Imani. Hakuna kanuni ya mipaka inayosema kuwa ni mitume tu au kanisa la kwanza tu ndio walioweza kupokea karama hii.

Wala hapana mpaka wa wakati uliowekwa juu ya Umwagwaji wa Roho Mtakatifu, alimradi tu Mungu anashughulika na wanadamu, hata wakati wa kurudi kwa Kristo kwa kanisa lake, Roho Mtakatifu amehaidiwa kwa watu.

KUNENA KWA LUGHA KULITABIRIWA KATIKA AGANO LA KALE

"La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa; ambao aliwaambia, Hii ndiyo raha yenu, mpeni raha yeye aliyechoka; huku ndiko kuburudika; lakini hawakutaka kusikia" (Isaya 28:11-12)

Yesu akasema "Njoni kwangu niyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha" (Mathayo 11:28).

ROHO MTAKATIFU AMWAGWA

"Wote wakajazwa Roho Mtakatifu wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka" (Matendo 2:4).

Hapa imetajwa kwa kudhihirishwa kuwa wanafunzi walipopokea Roho Mtakatifu walinena kwa lugha. Hii ilikuwa ni mara ya kwanza Roho Mtakatifu kutolewa. Huonyesha kama mfano kwa wale wanaofuata.

"Ndipo wakaweka mikono yao juu yao wakampokea Roho Mtakatifu. Hata Simoni aliona ya kuwa watu wanapewa Roho Mtakatifu kwa kuwekewa mikono kwa Mitume, akataka kuwapa fedha akisema, nipeni na mimi uwezo huu, ili kila mtu nitakayemwekea mikono yangu apokee Roho Mtakatifu" (Matendo 8:17-19).

Hili jambo la wasamaria kupokea ubatizo wa Roho Mtakatifu halitaji kunena kwa lugha nyingine. Hata hivyo linaelezea kwamba Simoni waliona kwamba walipokea Roho Mtakatifu. Simoni asimgekuwa yule ambaye wangelimwiita wa kiroho. Alijuaje basi kwamba walikuwa wamepokea Roho Mtakatifu? Kulikuwako na ushahidi uliomshawishi Simoni. Huo ulikuwa ni upi? kama ukisoma katika sura ile ya nane ya kitabu cha Matendo ya Mitume utaona kuwa Wasamaria tayari walishabatizwa, wakaona miujiza na ishara, pepo walitolewa, walipokea uponyaji, na walikuwa na furaha kubwa.

Mitume walipowawekea mikono kitu tofauti kilitokea ambacho kilimjulisha Simoni kuwa wamepokea Roho Mtakatifu. Kule Yerusalemu walinena kwa lugha walimpokea Roho Mtakatifu, Je haileti maana kumalizia kwa kusema kuwa walifanya hivyo pia kule Samaria?

"Anania akaenda zake, akaingia mle nyumbani, akamwekea mikono akisema Ndugu Sauli, Bwana amenituma, Yesu yeye aliyekutokea katika njia uliyojia upate kuona tena, ukajazwe Roho Mtakatifu, Mara vikaanguka machoni pake vitu, kama magamba, akapata kuona akasimama, akabatizwa" (Matendo 9:17-18)

Katika tukio hili haijaelezwa kuwa Paulo alinena kwa lugha alipompokea Roho Mtakatifu. Kwa ajili hiyo haielezi kuwa alimpokea Roho Mtakatifu, Ingawaje lazima tusikie kuwa huu ni wakati alipopokea ubatizo wake wa Roho. Anania alitumwa kwa kusudi lile. Tunafahamu kuwa baadaye katika kuongoka kwa Paulo alinena kwa lugha. Paulo alitoa tamko hili, "Namshukuru Mungu ya kuwa nanena kwa lugha zaidi ya ninyi nyote" (1 Wakorintho 14:18). Kwa hiyo, ingawaje haisemi kuwa Paulo alinena kwa lugha katika Matendo 9 tunatambua kuwa baadaye

alikuwa ni mnenaji kwa lugha mkubwa .

"Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliosikia lile neno. Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashangaa, watu wote waliokuwa pamoja na Petro, kwa sababu mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwa lugha na kumwadhimisha Mungu..." (Matendo 10:44-46).

Tena andiko linaeleza kwamba walinena kwa lugha walipompokea Roho Mtakatifu nyumba ya Kornelio walipokea Injili kwa mara ya kwanza na mlango ukafunguliwa kwa mataifa kushiriki ahadi ya kipawa cha Mungu.

"Na Paulo alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao: Wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri" (Matendo 19:6).

Tena imenenwa kwa uwazi kuwa walinena kwa lugha walipojazwa Roho Mtakatifu. Inastaajabisha kugundua kuwa katika kila sehemu wanapotaja kuwa walinena kwa lugha walipompokea Roho Mtakatifu, hakuna aliyeonekana kuuliza ni kwa nini. Katika kila sehemu haikufundishwa kwao kuwa jambo hili lingetokea. Hawakutegemea jambo hili na hata lilipotokea hawakuwa na mahoji. Lilikubalika kwa sababu ya Ushuhuda wa Roho. Kuna Ufahamu wa kiroho unaotokea kwa kupokea Ubatizo wa Roho Mtakatifu. Roho wake hushuhudia pamoja na roho zetu ya kuwa tu wana wa Mungu.

Kuna matukio matano katika Biblia ambapo ubatizo wa Roho Mtakatifu ulipokelewa. Mara tatu iliandikwa kuwa walinena kwa lugha. Hii imetolewa kama uthibitisho kwa wengine wasemao kuwa kunena kwa lugha si ushahidi muhimu wa kumpokea Roho Mtakatifu. Tutachunguza mwisho huu kwa maswali yafuatayo;
Je kuna mifano yoyote ya kimaandiko inayosema kuwa hawakunena kwa lugha walipompokea Roho Mtakatifu?

Je watatu kati ya watano waliompokea Roho Mtakatifu katika kanisa lako hunena kwa lugha? Kuna yoyote kati yao hunena kwa lugha?

Huwa kila anayempokea Roho Mtakatifu katika makanisa yenu wanafanya hivyo kwa ishara yenye kuonekana hapo hapo kwa wazi mbali na furaha, miujiza na kadhalika?(Kama walivyofanya Samaria).

Huwa yeyote anayempokea Roho Mtakatifu katika makanisa yenu hunena kwa lugha baadaye? (kama Mtume Paulo).

Kwa hakika hakuna mtu mwamini Biblia angekataa kukubali Ushahidi wa maandiko. Kama ni waaminifu tutatambua tukio la ki-Biblia na kuona kweli ile inayoelezewa.

Sasa kuna wengine wanaopinga kunena kwa lugha kuwa kama ni ishara ya kumpokea Roho Mtakatifu. Baadhi wanasema kuwa Mitume walinena kwa lugha kwa sababu ya uhitaji wa kuhubiria watu wa lugha nyingine. Wanamtumia Petro siku ile ya Pentekoste na Paulo katika safari zake Asia ndogo kama mfano wa jambo hili. Zipo kweli mbili zinazofanya bishano hili lisiwe la kweli kwanza hakuna tamko la kimaandiko kuonyesha kuwa Petro, Paulo au mwingine awaye yote alihubiri kwa lugha. Kukosa Ushahidi wa kimaandiko kutetea dai hili, lazima basi wachague mantiki. Ingawaje, mantiki inashindwa kusaidia wazo la namna hii. Kwanza kabisa, kama walihubiri kwa lugha katika kanisa la mwanzo, kwa nini hili halitokei leo? Wamisionari hutumia miezi au hata miaka kujifunza lugha na kwa kawaida kuhubiri kwa kumtumia mkalimali (Mtafsiri). Kwa hakika uhitaji ni mkuu leo kwa uwezo wa kuhubiri kwa lugha kama ilivyokuwa katika kipindi cha mitume. Hakika

ni kuwa ilikuwa siyo muhimu kwa mitume kuhubiri kwa lugha. Petro alipohubiri siku ile ya Pentekoste alikuwa anawahubiria wayahudi kutoka kila taifa chini ya mbingu. Hawa walikuwa ni Wayahudi wa kidini waliokwenda kwenye jambo kuu na gharama kuwa Yerusalemu kwa ajili ya Sikukuu ya Pentekoste. Je tuseme kuwa hawa Wayahudi wa dini hawakuelewa lugha yao wenyewe? Pia, ingekuwa ni muujiza halisi kwa Petro kuhubiri katika lugha kumi na tano kwa mara moja. Kwa sababu kulikuwa angalau watu wa mataifa hayo siku ile. Tena Biblia haiandiki muujiza kama huo. Kwa kweli, katika siku ya Pentekoste, walikuwa wananena kwa lugha hata kabla ya mkutano kukusanyika. Je walikuwa wanahubiriana wao kwa wao? Kama vile Paulo na wengine katika safari zao za utume, hali isiyo ya kawaida ilisaidia makubiri yao katika nchi za kigeni. Ulimwengu wa wakati uleulikuwa umetawaliwa na wa-Rumi, lakini mfumo wa utawala uliokuwa umetangulia wa ki-Giriki ilikuwa kiyunani ni lugha ya kawaida katika ulimwengu (Kiyunani). Agano Jipya liliandikwa na Wayahudi ila katika lugha ya . Popote mitume walikokwenda waliweza kuhubiri katika lugha ya Kiyahudi au ki-yunani. Hakukuwa na uhitaji wowote kwa wao kuhubiri kwa kunena kwa lugha, Mungu wetu ni mtenda miujiza, ila hutumia nguvu zake kwa makusudi hakukuwa na sababu iliyosababisha kuhubiri kwa lugha katika kipindi cha mitume.

Baadhi wamesema kuwa kunena kwa lugha kwa siku hizi kwa kweli, kuwa ni kupayuka tu. Mzigo wa kudhibitisha u mabegani mwao. Tungetaja mifano kadhaa wa matukio ambayo kunena kwa lugha kulitambulika kama lugha na hiyo nyakati hizi, Inasemekana kuwa mtu aliyeona tukio si sawa sawa na mtu anayebisha tu. Kuna lugha maelfu na mahojiano yanayozungumzwa Ulimwenguni leo. Kila mojawapo ya lugha hizi zina maendeleo ya kukua. Ingekuwa ni vigumu sana, kwa mfano, kwa wale wasioanzisha kutambua kiingereza kinachozungumzwa katika vipindi vya kati. 1 Wakorintho 13:1 hutaja lugha za malaika. Mtu anayetaka kuthibitisha kuwa kunena kwa lugha ni kupayuka tu ana kazi ngumu kwa kweli.

Imekuwa ikiulizwa kwa ambao wamesha nena kwa lugha: Kitu gani kimatokeo kwa upepo na kumwagwa kwa Roho Mtakatifu siku ya Pentekoste? Kwa nini dhihirisho hizi hazionekani leo? Kama ishara ya kujazwa Roho Mtakatifu, basi mbona hatuoni Upepo na moto? Kwanza kabisa, Inatupasa tukumbuke kuwa sauti kama Upepo uvumao, na ndimi kama za moto kwa hakika zilitokea kabla ya kujazwa Roho Mtakatifu. Hapa tunashughulikia kinachotokea baada ya kumpokea Roho Mtakatifu, si kabla kama tungehitaji kuwa tuende tukaombe kule Yerusalemu katika siku ya Pentekoste. Upepo na moto katika Matendo 2:2-3 ni sawa na wingu lile lililoufunika mlima na sauti kama ya ngurumo iliyokuja kabla ya kutolewa sheria. Hizi zilikuwa ni ishara za Uzinduzi zilizoonyesha tukio lililokuwa karibu kutokea. Baada ya Sheria kutolewa, wingu na sauti havikutokea tena, kwa mara ya pili. Ingawaje, sheria ilikuwapo bado. Siku ya 20 mwezi wa kwanza baada ya kila miaka minne tunamsimika Raisi wa Marekani. Hili ni tukio maalumu la pekee katika kipindi chake cha miaka minne, ila yeye ni Raisi kila siku ya kipindi chake, hata pasipo sherehe ya Uzinduzi kurudiwa tena. Kuzaliwa na huduma ya Yesu vyote vilikuwa na matangazo ya Uzinduzi: Malaika katika kuzaliwa kwa Yesu na sauti ya Mungu katika Ubatizo wake. Mungu ameamua kufanya mambo kwa njia hii. Ni kwa kawaida tu kuwa ishara za Uzinduzi za upepo na moto havirudiwi leo. Na pia hatuoni vikitokea tena katika matukio ya baadaye ya wengine wanaompokea Roho Mtakatifu. Ingawaje, tunaona muujiza wa kusikia kwa lugha unatokea tena.

Kunena kwa lugha siyo ishara ya uzinduzi, ila ushahidi wa jambo ambalo tayari limesha tokea.

Bishano lingine limetolewa, Ingawaje ni dhaifu sana: kuwa kunena kwa lugha ulikuwa siyo muujiza wa kunena bali muujiza wa kusikia: "Imekuwaje basi sisi kusikia kila mtu lugha yetu tuliyozaliwa nayo?" (Matendo 2:8). Mstari huu wa mawazo unakutana na mambo magumu, Ingawaje, kwanza, katika andiko hapo juu wasikilizaji walitengana na walikuwa wa mwilini. Mungu hatendi muujiza katikati ya kusanyiko la aina hiyo. Angewapitaje wanafunzi wake mwenyewe waliokuwa wanamwabudu yeye kwa Umoja na kutenda muujiza kuwa tumia watu waliogawanyika na waliochanganyikiwa? Jambo la pili andiko linasema kuwa walinena kwa lugha (Matendo 2:4). Tena kama lugha ni muujiza wa kusikia, kwa nini ujumbe katika lugha huhitaji kutafsiriwa? Kwa nini Mungu asiache tusikie kile alichotaka kusema mara ya kwanza? Mwisho, Isaya 28:11-12 inaeleza kabla kuhusu midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine, si maalumu kwa masikio yenye upako.

Tukipewa umuhimu mkubwa wa Roho Mtakatifu kwenye wokovu wetu na kutembea kwetu baadaye na Mungu ni muhimu kwetu sisi kuhakikisha kuwa kwa hakika tumezaliwa kwa Roho wake. Hii inaitwa nguvu kwetu kwa hakika kuwa Mungu Ametupa ishara dhahiri ya kunena kwa lugha, Swali tunalohitaji kujiuliza ni lile ambalo Paulo aliwauliza wanafunzi wa Yohana kule Efeso. "Je mlimpokea Roho mtakatifu mlipoamini?"

WOKOVU MIFANO NA VIVULI

"Lakini kabla ya kuja ile imani tulikuwa tumewekwa chini ya sheria, tumefungwa mpaka ije ile imani itakayofunuliwa, Hivyo Torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo" (Wagalatia 3:23-24).

"Basi torati kwa kuwa ni kivuli cha mema yatakayokuwa, wala si sura yenyewe ya mambo hayo, kwa dhabibu zile zile wanazozitoa kila mwaka daima haiwezi wakati wowote kuwakamilisha wakaribiao." (Waebrania 10:1)

Wokovu wetu ni kusudi zima la maandiko. Kudumu ndani ya maelezo ya mashujaa wa Imani ni dhana za wokovu wetu. Katika marudio ya kuchosha ya kumbukumbu ni sheria zilizo onyesha kabla ukombozi wetu. Nabii hazikueleweka vizuri hata na wale waliozisema zikingaa kama nguzo ya moto kutuongoza kwenye uzima wa milele. Katika vifungu vifuatavyo chache ya lulu hizi za thamani zinafunuliwa ili tustaajabu mpango wa Mungu wenye kupendeza na kutambua ukweli na usahihi wa njia ya kuuendea Ufalme wa Mungu.

DESTURI ZA NDOA ZA WAYAHUDI

Swala la ndoa lilikuwa ni jambo muhimu kwa Wayahudi wa siku za Yesu. Taifa dogo Wayahudi walilichukulia kwa makini suala la kuongeza idadi yao ya watu. Ndoa ilikuwa ni wajibu wa mwanamume na tegemeo pekee la mwanamke. Katika kitabu cha mafundisho cha Wayahudi swali linauliza, "Ni muda gani ulimchukua Mungu kuumba ulimwengu?" Jibu, "Siku sita na siku ya saba alistarehe"

Hii ilifuatiwa na swali, "Amekuwa akifanya nini tokea wakati huo? Pasipo kusita jibu likatokea, "Kupanga Ndoa."

Kijana wa miaka ishirini au zaidi alikuwa akikemewa hadharani kama hakufanya mipango makini ya ndoa katika siku zake za mapumziko. Motisha ya likizo ya mwaka mmoja kutofanya kazi na shughuli za kiserikali ilitolewa kwa mtu yeyote ambaye angeoa.

"Mtu aliyeoa mke mpya, asiende vitani pamoja na jeshi, wala asipewe shughuli juu yake yoyote: akae faragha mwaka mmoja nyumbani mwake, apate mfurahisha mkewe aliyemwoa" (Kumbukumbu la Torati 24:5).

Tumaini la Israeli lilikuwa ni masihi, Ambaye angelizaliwa kati yao.

"Maana kwa ajili yetu mtoto amezaliwa, Tumepata mtoto mwanamume: Na uweza wa Kifalme utakuwa begani mwake, Naye ataitwa jina lake, Mshauri wa ajabu, Mungu mwenye nguvu, Baba wa milele, Mfalme wa amani" (Isaya 9:6).

Yote haya hujumuishwa kufanya desturi zinazohusu ndoa jambo muhimu sana. Hakukumbukwa kuwa muujiza wa kwanza kuandikwa wa Yesu haikuwa kufufua wafu au kumfanya kilema kutembea. Muujiza wake wa kwanza wa kugeuza maji kuwa divai ulikuwa kwa kusudi la kutoa kwa ajili ya karamu ya Arusi.

Wazo la Kibiblia la Kanisa kama Bibi Arusi wa Kristo pamoja na karamu ya mwana kondoo iliyopigiwa mbiu sana inajumuisha kufanya somo la ndoa kuwa mpango kamili kwa Mungu kutumia kielelezo kwa ajili yetu mpango wake kwa wokovu wetu.

Kama katika taratibu nyingi za namna hiyo Wayahudi walizoea kuandaa Arusi. Baada ya Bwana harusi kumchagua bibi harusi mtarajiwa, angewatuma marafiki aliowaamini kutembelea nyumbani kwa wazazi wa Bibi harusi. Ilikuwa ni hawa marafiki waliofanya maandalizi ya Ndoa kwa uwazi sana, hii ni mbinu ile ile ambayo Kristo amelichumbia kanisa lake. Kama Paulo alivyosema:

"Basi tu wajumbe kwa ajili ya Kristo, kana kwamba anavyosema Mungu anasihi kwa vinywa vyetu, twawaomba ninyi kwa ajili ya Kristo mpatanishwe na Mungu" (2 Wakorintho 5:20).

"Maana nawaonea wivu, wivu wa Mungu, kwa kuwa nawaposea mume mmoja, ili nimletee Krist bikira safi" (2 Wakorintho 11:2).

Inatakiwa ijulikane kuwa, isivyofanana na kutokuelekea kwa desturi ya watu wa jamii ya wa-magharibi kuhusina na maandalizi ya harusi, msichana huwa na uchaguzi. Ingawaje desturi inafanya kuwezekana kushinikiza dai lake uso kwa uso, wazazi walikuwa ndio mawakala wa kufanya mkataba, binti alikuwa na nguvu ya veto (nguvu ya maamuzi ya hoja). Kwa jinsi hiyo hatujamwona uso wake. Tumepata tu habari zake kwa kupitia wajumbe wake wenye kuaminika wengine watafanya maombezi kwa ajili yetu, kutushuhudia, kututia moyo kumpigia kura yetu Bwana lakini hatimaye uchaguzi ni wetu.

Mara uamuzi unapokuwa umetolewa kulikuwa hakuna kurudi nyuma. Chumba zilichukuliwa kwa makini sana kati ya Wayahudi ikitakiwa gharama ya kuachana ili kuvunjwa. Kama posa zingevunjwa, ilikuwa ni kwa nadra sana, kwa maswala yasiyoweza kuzuilika, kama vile Yusufu alivyoazimia kwa Mariamu. Tabia ya Bibi arusi mtarajiwa ilikuwa ni kuwa posa iliashiria wajibu wa maisha kwa mume mtarajiwa. Inachukua uchunguzi wa uangalifu sana wa maandiko kutafuta mfano wa uchumba uliovunjika na hivyo kufanyika kwa ujanja. Mara tunapoamua

kumfuata Yesu, pasipo na wazo la kurudi nyuma.

Mojawapo ya sehemu muhimu sana ya posa ilikuwa ni utoaji wa zawadi kwa bibi arusi mtarajiwa. Yesu ametimiza jambo hili kwa karama ya Roho Mtakatifu na pia kwa baraka nyingi Alizozionyesha kwa kanisa lake. Hizi ishara ni ahadi za posa pamoja na ahadi ya mengi zaidi yaliyokuwa yaja.

Jambo lingine lililotimizwa katika posa ilikuwa ni Bibi harusi kuchukua jina la Bwana harusi. Hakusubiri harusi ili afanye jambo hili, katika posa alichukua jina la Bwana harusi na alikuwa na mamlaka ya kulitumia. Inashangaza namna gani kuona hili likitimizwa katika tukio la wokovu wetu wenyewe! Kwa ubatizo katika jina la Yesu Kristo tunaitwa kwa jina lake.

"Simoni ametueleza jinsi Mungu hapo kwanza alivyowaangalia mataifa ili achague watu katika hao kwa ajili ya jina lake" (Matendo 15:14).

Suala la ubatizo pia lilionyeshwa kabla katika Mikveh ni chemchemi ya kubatizia kwa kuwaosha waongofu wapya wa imani ya Kiyahudi na pia kwa sherehe ya utakaso wa bibi arusi mtarajiwa. Ilikuwa ni muhimu kwa maandalizi kwa ajili ya Arusi. Katika sherehe hii ya kuoshwa ya Mikveh bibi arusi mtarajiwa alitakiwa kuzamishwa kabisa kama maandalizi ya utakaso ili kutolewa kwa bwana harusi katika harusi. Ilikuwa haifikiriki kuingia katika harusi pasipo utakaso huu. Maandalizi ya harusi yasingeendelea pasipo jambo hili.

Hili ni jambo la kukumbuka la jaribio ambalo mtumishi wa Abrahamu alimpa Rebeka, Alitumwa na bwana wake kumtafutia Isaka bibi arusi, Aligundua jaribio kupambanua roho ya mwanamke kijana aliyemwona, alikutana na Rebeka kisimani. Akiwa na kiu kwa ajili ya safari ndefu, alimwomba maji, Hili lilikuwa ni ombi la kawaida kabisa ambalo kwa mara chache lingekataliwa. Ingawaje huyu mtumishi aliomba kama huyu binti alikuwa ni bibi arusi wa baadaye wa Bwana wake Isaka, kuwa angefanya zaidi ya ile kazi na pia kuwapa ngamia wake maji pia. Alifanya hivi na ikaonyesha kuwa ndiye aliyechaguliwa. Biblia inasema kuwa tunaokolewa kwa maji. Wengi wanahisi kuwa ubatizo si muhimu kwa wokovu. Hata hivyo hii isingedhihirisha roho ya bibi arusi kuridhika kutimiza suala hili la ubatizo? Kwa kufanya hivi tutaonyesha roho ya bibi arusi na pia kukubalika.

Baada ya kamilisho la posa Bwana arusi huendoka na akimwacha bibi Arusi; kuurudi nyumbani mwa baba yake. Hapa alitakiwa aandaye mahali kwa ajili ya bibi arusi wake na yeye mwenyewe kuishi pamoja.

"Nyumbani mwa baba yangu mna makao mengi: kama sivyo, ningaliwaambia: maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo" (Yohana 14:2-3).

Desturi ilikuwa ni kuwa mara baada ya mambo yote kukamilika, bwana arusi angerudi kumtaka bibi arusi wake. Hakutoa tamko kabla la kurudi kwake. Bibi harusi alitakiwa kuwa tayari kwa wakati wote kwenda pamoja naye.

"Nanyi jiwekeni tayari kwa kuwa saa msiyodhani ndipo ajapo mwana wa Adamu" (Luka 12:40).

Yote haya yanaonyesha kabla kurudi kwa Yesu Kristo kwa bibi harusi wake kanisa.

"Lakini usiku wa manane pakawa na kelele, Haya bwana arusi tokeni mwende kumlaki" (Mathayo 25:6).

Hapa Biblia inatupa mfano wa kurudi Bwana arusi. Usiku wa manane alikuja tu na tangazo la ghafla linalokuja nyuma yake. Pasipo kusita bibi arusi aliitikia. Alikuwa amejiandaa, haikufikirika kumwacha asubiri, au kumwacha yeye aifikie nyumba yake (bibi arusi) Alitoka nje kumlaki.

"Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tulio salia, tutafanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki bwana hewani: na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele" (1 Thesalonike 4:16-17).

Kwa kuzungumza kuhusu wanawali wenye busara na wapumbavu walioitwa kwenye sherehe ya arusi. Biblia inatueleza kuhusu uhitaji wao wa taa. Taa hazikukusudiwa tu kumulika njia. Zaidi ya lile, zilikuwa za kupamba sikukuu, zilikusudiwa kuwa ni sehemu ya sherehe. Ilikuwa haifikiriki kufika shereheni pasipo kuongeza mng'ao wa tukio.

Kuruhusu mafuta ya Roho Mtakatifu kupunguka hivyo tunakosa furaha ya wokovu wetu haiwezi kufikiria kabisa.

"Hayo nimewaambia, ili furaha yangu iwe ndani yenu, na furaha yenu itimizwe" (Yohana 15:11).

Baada ya kuwasili kwenye karamu ya arusi inatakiwa kuvaa vazi maalumu la harusi.kwa kwa sababu alikuwa hajavaa vazi la harusi. Hii inaonekana ni ukali sana mpaka ujue desturi. Ilikuwa ni kwa desturi kwa bwana harusi kutoa vazi la harusi kwa kila mmoja aliyefika harusini, ili pasiwepo tofauti kati ya tajiri na maskini. Hivyo hakukuwa na sababu kwa mtu yeyote kuwa pale pasipo vazi la arusi. Kukataa kuvaa vazi la arusi kulisababisha kutolewa karamuni. Inahisiwa sana kuwa hili vazi la arusi ni haki ya watakatifu. Biblia inasema haki yetu ni kama matambara mabovu. Ingawaje, tunaweza kupata manufaa ya neema yake.

Katikati ya karamu, upeo wa arusi ulifikia. Yeye hutoa vazi la haki ili kwamba tuweze kuingia ndani. Bibi arusi ambaye alikuwa amefunikwa kabisa mpaka wakati huu aliingia katika chumba cha ndani pamoja na bwana arusi, ambao walifunga mlango. Nje ya mlango rafiki wa bwana arusi walisubiri, kuisikiliza sauti ya bwana arusi.

"Aliye naye bibi arusi ndiye bwana arusi lakini rafiki yake bwana arusi yeye anayesimama na kumsikia, aifurahia sana sauti yake bwana arusi. Basi hii furaha yangu imetimia" (Yohana 3:29).

Desturi ilikuwa ni kwamba bwana arusi angeondoa shela toka kwa bibi arusi, na kwa mara ya kwanza angeuona uzuri wake. Furaha yake ya kuona uzuri wa bibi arusi wake ulimsababisha kupaza sauti ya furaha, ambayo ilipokelewa na rafiki zake.

"...na kama vile bwana arusi amfurahiavyo bibi arusi ndivyo Mungu wako atakavyokufurahia wewe" (Isaya 62:5).

Ni furaha iliyoje wakati pazia linapoondolewa ndani ya kanisa kwa kuwa wakati wetu wote tumekuwa tukifunikwa katika kushindwa mwili wenye uharibifu. tumekuwa tukiona kama kwa kupitia kioo cheusi, pasipo kutambua halisi utukufu wa Mfalme wetu anayekuja. Ila ahadi ni kuwa siku moja huu uharibikao utavaa kutokuharibika, na tutamwona kama alivyo, kwa wakati huo huo, Kristo atatazama kwa mara ya kwanza uzuri dhahiri na Utukufu wa Bibi arusi wake, kanisa, Haishangazi anakuja na shangwe, si ya ushindi tu, ila ya unyakuo kamili katika

matunda ya kazi yake. mateso na pendo. oo ametupenda kiasi gani.

"Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko na sauti ya malaika mkuu na parapanda ya Mungu..." (2 Thesalonike 4:16).

Kama vile bibi arusi atazamiavyo siku yake ya arusi, tunatazamaia kwa shauku si siku za mbali sana wa kati bwana wetu anarudi kutuchukua kwenda kwake.

"Yeye mwenyewe kuyashuhudia haya asema, naam: naja upesi, Amina; na uje Bwana Yesu" (Ufunuo 22:20).

ADAMU NA KRISTO

KUFANANA NA UTOFAUTI

Vyote kufanana na tofauti za Adamu na Yesu hutumika kuangaza mpango wa kupendeza wa Mungu wa wokovu wetu.

"Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika kristo wote watahuishwa" (1 Wakorintho 15:22).

Tofauti kati ya Adamu na Yesu hutuonyesha sisi tofauti kati ya wa duniani na wa mbinguni.

"Ndivyo alivyoandikwa, mtu wa kwanza Adamu akawa nafsi iliyo hai; Adamu wa mwisho na roho yenye kuhuisha. Na kama tulivyochukua sura yake yule wa udongo, kadhalika tutaichukua sura yake yeye aliye wa mbinguni" (1 Wakorintho 15:45, 49).

Kutambua tofauti kati ya wa dunia na wa mbinguni ni muhimu sana kwa maendeleo yetu kiroho.

"Kwa kuwa nia ya mwili ni mauti: bali nia ya roho ni uzima wa amani" (Warumi 8:6).

Uadui ulioelezewa na Paulo katika Warumi mlango wa saba ni mapambano tofauti kati ya mwili na roho. Paulo alitoa maoni kuhusu hiki kizuizi kisichoepukika cha mwili na akapaza sauti kusema "Ole wangu, ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti," Jibu kwa lile swali linatuonyesha kiini cha Ushindi. "Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu."

“Sasa, basi, hakuna hukumu ya adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu” (Warumi 8:1).

“Walakini mauti ilitawala tangu Adamu mpaka Musa, nayo iliwatawala hata wao wasiofanya dhambi ifananayo na kosa la Adamu, aliye mfano wake yeye atakaye kuja" (Warumi 5:14).

Kufanana kwa Adamu na Kristo kunatuonyesha pendo kuu ambalo Kristo alikuwa nalo kwa ajili ya kanisa.

Kutokana na tukio la maandiko tunajiuliza kuwa Hawa alianguka kwa sababu alidanganywa. Adamu ingawaje, aliingia katika kosa macho yake yakiwa wazi yamefunguka.

"Wala Adamu hakudanganywa, ila mwanamke alidanganywa kabisa akaingia katika hali ya kukosa" (1 Timotheo 2:14).

Inaweza kutufanya tushangae kwa nini Adamu alianguka. Hakudanganywa, kwa sababu huyo aliingia katika kosa akijua kuwa alikuwa anashiriki dhambi na akijua uhakika wa hukumu itakayokuja. Kwa kutafuta motisha inayowezekana kwa uamuzi wake, Sababu moja tu yenye kujipendekeza huja akilini; Pendo lake kwa

Hawa. Je siyo sababu kudhani kuwa kwa sababu ya pendo lake kwa mke wake Adamu alikuwa radhi kushiriki katika kosa? Kwa kutotaka kutengwa na mpenzi wake alionja tunda chungu la dhambi.

"Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwa ajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika yeye" (2 Wakorintho 5:21).

"Sisi sote kama kondoo tumepotea; kila mmoja wetu amegeukia njia yake mwenyewe: Na Bwana ameweka juu yake maovu yetu sisi sote" (Isaya 53:6).

Kwa sababu hakutaka kutengwa na mpenzi wake, Yesu alionja kikombe kichungu cha dhambi na akahesabiwa pamoja na wakosa, kwa dhabihu hii kubwa yake Yeye mwenyewe aliweza kumkomboa bibi arusi wake."

UUMBAJI NA WOKOVU

"Maana tu kazi yake, tuliumbwa katika Kristo Yesu, tutende matendo mema, ambayo tokea awali Mungu aliyatengeza ili tuenende kwayo" (Waefeso 2:10).

Tukio la uumbaji ni mpango mwingine wa kupendeza kwa kuonyesha kielelezo cha mpango wa Mungu wa wokovu. Kuchukua machafuko na mafarakano na kuleta uzima na mpangilio ni hatua hakika inayotusafirisha toka gizani kuelekea nuruni. Maelezo ya kimaandiko hutupa siku kwa siku mfuatano wa matukio ambayo kwa hakika yanaendana na Ukombozi wetu.

"Hapo mwanzo Mungu aliziumba mbingu na nchi. nayo nchi ilikuwa ukiwa, tena utupu, na giza lilikuwa juu ya uso wa maji. Mungu akasema, iwe nuru; ikawa nuru, Mungu akaiona nuru, ya kuwa ni njema. Mungu akatenga nuru na giza" (Mwanzo 1:1-4).

Tunaujia wokovu toka giza la kiroho. Hali ya vita katika mwanzo wa uumbaji ni uchambuzi kamili wa dhambi jinsi tunavyoweza kufikiri. Watu waliopotea wa Ulimwengu huu wanaishi katika giza, kuchanganyikiwa, na Utupu. Tukio la kwanza kabisa katika safari yetu toka ufalme wa shetani kuelekea Ufalme wa Mungu ni mng'ao wa ajabu wa nuru ya Mungu, katika mioyo yetu ya giza kwa kufumbuliwa macho yetu na kuijua kweli tunajulishwa hali yetu ya Upotevu. Kama nuru ilivyotengwa na giza, kweli inatofautishwa na kosa ili tupate kuamua kati yake. Tukiwa na nuru ya kutuongoza tunaweza kuona njia yetu kutokana na mtego wa shetani. Nuru hii inatujia kwa kulisikia neno la Mungu.

"Watu wale waliokwenda katika giza wameona nuru kuu; wale waliokaa katika nchi ya uvuli wa mauti, Nuru kuu imewaangaza" (Isaya 9:2).

Siku ya pili ya uumbaji inaelezea hatua za kuendelea na utengaji na umakini katika kuumba Ulimwengu mpya.

Mungu akasema, Na liwe anga katikati ya maji, likayatenge maji na maji. Mungu akalifanya anga akayatenga yale maji yaliyopo juu ya anga na yale maji yaliyo chini ya anga; ikawa hivyo" (Mwanzo 1:6-7).

Swala la kutenga maji na kuweka Mtengano mkubwa kabisa kati ya wa duniani na wa mbinguni inaelezea uhakika wa toba.

"Kwa hiyo, tokeni kati yao, mkatengwe nao, asema Bwana, Msiguse kitu kilicho kichafu, Nami nitawakaribisha..." (2 Wakorintho 6:17).

Siku ya tatu Mungu tumeona akiileta ardhi kutoka maji yaliyoifunika. Uhai ukatokea kwa mara ya kwanza.

"Mungu akasema, maji yaliyo chini ya mbingu na yakusanyike mahali pamoja ili pakavu paonekane: Ikawa hivyo, Mungu akapaita pale pakavu nchi na makusanyiko ya maji akayaita bahari: Mungu akasema, Nchi na itoe majani, mche utoao mbegu, na mti wa matunda uzaao matunda kwa jinsi yake, ambao mbegu zake zimo ndani yake, juu ya nchi: ikawa hivyo" (Mwanzo 1:9-11).

Nini tena hili linaweza kutueleza isipokuwa ni muujiza wa ubatizo? Tunatoka katika maji ya Ubatizo kuendea upya wa maisha.

"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya Utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima" (Warumi 6:4).

Mwanzo 1:14-15 inatupa tukio la uumbaji wa jua, mwezi na nyota. "Mungu akasema, na iwe mianga katika anga la mbingu ili itenge kati ya mchana na usiku; nayo iwe ndiyo dalili na majira na siku na miaka: tena iwe ndiyo mianga katika anga la mbingu itie nuru juu ya nchi; Ikawa hivyo."

Haya yaliwekwa ili kutoa mwelekeo na kuweka wakati kwa hii inamaanisha isiyo na njia na mamajusi waliifuata nyota kumtafuta mtoto Yesu.

Hii inatukumbusha kuwa tunapoanza maisha mapya ndani ya Kristo, inatupasa tutembee nuruni, kama Yeye alivyo nuruni. Tumepewa neno la Mungu kama kiongozi kwa safari yetu kuingia ufalme wa Mungu.

"Neno lako ni taa ya miguu yangu, na mwanga wa njia yangu" (Zaburi 119:105).

"Mungu akasema, maji na yajae kwa wingi na kila kitu kiendacho chenye uhai na ndege warukao juu ya nchi katika anga la mbingu. Mungu akaumba nyangumi wakubwa, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho, ambavyo maji yalijawa navyo kwa wingi kwa jinsi zao,na kila ndege arukaye, kwa jinsi yake: Mungu akaona ya kuwa ni vyema" (Mwanzo 1:20-21).

Siku ya tano ya hatua ya uumbaji inatoa viumbe hai vya kwanza nje ya maji. Samaki, ndege na wanyama wanatokea, wakitoa mlio hai wa kwanza.

Mtoto mdogo anapozaliwa kuwa na kipindi kifupi cha shauku ni kusubiri kilio cha kwanza cha mtoto. Hiki kilio kinaonyesha kuwa uhai umepuliziwa ndani ya mtoto.

"Kwa kuwa hamkupokea tena roho ya utumwa iletayo hofu, bali mlipokea roho ya kufanywa wana, ambayo kwa hiyo twalia Aba, yaani Baba" (Warumi 8:15).

Uzao wa Roho huwa unatambuliwa na sauti ya kunena kwa lugha.

"Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajilia kutamka" (Matendo 2:4).

Siku ya sita mtu aliumbwa katika sura ya Mungu. Agizo lilitolewa la kuzaana na kuongezeka.

"Mungu akasema, na tumfanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu, wakatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na wanyama, na nchi yote pia, na kila chenye kutambaa kitambaacho juu ya nchi. Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimuumba, Mwanamume na mwanamke aliwaumba, Mungu akawabarikia, Mungu akawaambia, Zaeni mkaongeze, mkaijaze nchi, na kuitiisha: mkatawale samaki wa baharini, na ndege wa angani, na kila kiumbe chenye uhai kiendacho juu ya nchi" (Mwanzo 1:26-28).

Ukombozi uzao mpya, kukua kiroho na ushindi vyote vimeonyeshwa kabla katika hii siku ya sita. Matokeo ya mwisho ya mpango wa Mungu ni kuwa

tutafanana naye. Kufikia mfano wake ni lengo la kila mtoto wa Mungu.

Kwa kuzaa tunda la Roho tunakua zaidi na zaidi katika mfano wake. Kwa kushikisha tukio na kukuza kanisa. Kushinda majaribu na kumshinda shetani kunaashiria nguvu tuliyopewa kutawala.

"Na siku ya saba Mungu alimaliza kazi yake yote aliyoifanya: akastarehe siku ya saba, akaacha kufanya kazi yake yote aliyoifanya" (Mwanzo 2:2).

Kwa hakika Kristo ni pumziko letu.

"La, bali kwa midomo ya watu wageni, na kwa lugha nyingine atasema na watu hawa: ambao aliwaambia, Hii ndiyo raha yenu, mpeni raha yeye aliyechoka, huku ndiko kuburudika..." (Isaya 28:11-12).

"Njoni kwangu ninyi nyote msumbukao na wenye kulemewa na mizigo, nami nitawapumzisha" (Mathayo 11:28).

HEKALU

"Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala ninyi si mali yenu wenyewe: maana mlinunuliwa kwa thamani. Sasa basi, mtukuzeni Mungu katika miili yenu" (1 Wakorintho 6:19-20).

Tunapofikiria kuhusu hekalu tunafunua sura za kuabudu dhabihu za matoleo, Utakaso na maombi. Hizi ni aina ya shughuli zinazotakiwa kutokea katika hekalu. Sheria ya kiroho kumtukuza Mungu katika miili yetu inatuambia namna ya kushughulikia mambo ya mahekalu yetu. Hakika kutambua matukio yanayolizunguka hekalu letu kunaweza kutusaidia kufahamu vizuri wokovu wetu wenyewe.

Mlango wa sita wa wafalme wa 1 unaelezea Utukufu wa hekalu lililojengwa na Sulemani. Lilijengwa kiajabu sana na kufanywa na vitu vyenye thamani kubwa.hakuna gharama iliyohifadhiwa kwa kuleta mienenzi ya Lebanoni, kazi ya mawe ilifanywa kabla ya jiwe kuletwa katika mahali pa ujenzi, Michoro ya kupendeza iliandaliwa na dhahabu ya kutosha. Hekalu lililojengwa na Suleimani kwa hakika lilikuwa ni mojawapo ya maajabu ya dunia, Kamilifu na kupendeza. Vyote hivi ni Kumtukuza Mungu wa hekalu. Katika 1 Wafalme tunasoma kuhusu michoro ya kupendeza iliyowekwa juu ya nguzo za shaba kama miguu thelathini kwenda juu, ambapo ilikuwa ni vigumu macho ya mwanadamu kuona. Hii ilifanyika kwa kmufurahisha Mungu, kama tunavyobadilisha mara nyingi maisha yetu katika njia ambazo watu wasingegundua, ila tunafanya ili kumpendeza Mungu.

Fahali ishirini na mbili elfu na kondoo laki moja na ishirini elfu vilitolewa kama sadaka za amani katika kuliweka Wakfu hekalu (1 Wafalme 8:63). Fahari ya namna hii haikujulikana kabisa kabla katika Israeli, wala haijaonekana kabisa baada ya hapo. Hili hekalu lilikuwa la tofauti hakika na utajiri. Hakuna lililofuatia ambalo lingeweza kufananishwa nalo.

Yote haya yalisisitizwa na roho nzuri ya Suleimani kadri alivyoweza. Maombi yake ya Wakfu ni Ushuhuda wa Kupendeza wa Unyenyekevu na shauku yenye bidii kumpendeza Bwana ambao ulikuwa ni moyo wa Mfalme Suleimani hapo mwanzo. Aliomba msamaha na kuwa Bwana angeliweka Jina lake hekaluni. Suleimani alitambua katika 1 Wafalme 8:27 kuwa hata ile nyumba kubwa aliyojenga

haikutosha na haikuwa inastahili kuwa makazi ya Yehova. Juhudi hizo hazikupita bila kujulikana na Bwana wetu.

"Ikawa makuhani walipokwisha kutoka katika patakatifu; (Kwani makuhani wote waliokuwepo walikuwa wamejitakasa, wala hawakuzishika zamu zao; tena walawi wa imbaji, wote pia, yaani Asafu na Hemani, na Yeduthuni, na wana wao, na ndugu zao, hali wamevaa kitani safi, wenye matoazi na vinanda na vinubi wamesimama upande wa mashariki wa madhabahu na pamoja nao makuhani mia na ishirini wakipiga panda) hata ikawa wenye panda na waimbaji walipokuwa kama mmoja, wakisikiliza sauti moja ya kumsifu na kumshukuru Bwana; nao wakipaza sauti pamoja na Panda na matoazi na vinanda, wakimsifu Bwana, wakisema, kwa kuwa ni mwema ; kwa maana fadhili zake ni za milele; nyumba ya Bwana, hata makuhani hawakuweza kusimama ili kufanya huduma yao, kwa sababu ya lile wingu; kwa kuwa nyumba ya Mungu imejaa utukufu wa Bwana" (2 Nyakati 5:11-14).

Uzuri na Utukufu wote wa hekalu la Suleimani, Ingawaje, haukuweza kuvumilia mkono wa kushindwa na kifungo kilichofuata kilicholetwa na dhambi.

Ahadi za Mungu wakati wote ni za masharti, na dhambi ya Israeli ilitangua ahadi zote za hekalu la mwanzo. Mateso ya kifungo katika nchi ya mbali ya mataifa mwishowe iliirudisha Israeli katika fahamu zake: Safari ilifanywa kuelekea Yerusalemu tena na hekalu likasimamishwa toka majivu.

Hekalu ambalo Mungu alimtumia Zerubabeli kujenga lilikuwa ni kumbukumbu ya toba na kurejeshwa upya katika Yerusalemu. Wakati ulipofika kwa hili hekalu kuwekwa Wakfu, Vijana walifurahi kwa ushindi wao, wakati wazee walioliona hekalu la Suleimani walilia kwa kuyalinganisha haya mawili.

"Miongoni mwake amebaki nani aliyeiona nyumba hii katika utukufu wake wa kwanza? nanyi mnaionaje sasa? Je mbele ya macho yenu, siyo kama si kitu?" (Hagai 2:3)

Mahali Suleimani alipoweka dhahabu Zarubabeli aliweka shaba. Shauku ya Suleimani kulijenga hekalu ilibadilishwa na matamshi makali ya nabii Hagai kuweka kando kupuuza kwao na kujenga nyumba ya Mungu. Hapajatajwa makundi makubwa mno ya kondoo na fahali yaliyoletwa kwa ajili ya dhabihu. Uzuri na Utukufu wa hekalu la mwanzo ulionekana kuigwa kwa juhudi zao hafifu. Ila Mungu kwa Rehema zake hakujali kama hekalu lao lilikuwa limefifia kwa sababu alijua kuwa uwepo wake mwenyewe ulitosha kuling'arisha.

"Nami nitatikisa mataifa yote, na vitu vinavyotamaniwa na mataifa yote kuja. nami nitaijaza nyumba hii utukufu, asema Bwana wa majeshi. Fedha ni mali yangu, na dhahabu ni mali yangu, asema Bwana wa majeshi. Utukufu wa nyumba hii utakuwa mkuu kuliko utukufu wake wa kwanza, asema Bwana wa majeshi; na katika mahali hapa nitawapa amani asema Bwana wa majeshi" (Hagai 2:7-9).

Tukirudi 1 Wakorintho 6:19-20 tunakumbushwa kuwa mwili ni hekalu la Roho Mtakatifu. Hii inatuleta kwenye kufananisha ambako kuna umuhimu sawa na mahekalu ya Suleimani na Zerubabeli: Nafsi za Adamu na Kristo.

"Mungu akasema, Na tufanye mtu kwa mfano wetu, kwa sura yetu; wakatawale..." (Mwanzo 1:26).

"Mungu akaumba mtu kwa mfano wake, kwa mfano wa Mungu alimwumba mwanamume..." (Mwanzo 1:27).

"Mungu akaona kila kitualikichokifanya, na tazama, ni chema sana..."

(Mwanzo 1:31).

Hili tukio la kuumbwa kwa Adamu haliachi mashaka kama vile ukamilifu wa kibinadamu aliokuwa nao. Aliumbwa kwa mfano wa Mungu, akathibitishwa na Mungu pasipo unajisi wa dhambi kuharibu sura yake, hakuwa na kosa. Ingawaje haiwezekani kumfananisha Adamu na vizazi vingine vilivyofuata, hakuwa na mashaka alikuwa mtu mkamilifu kabisa aliyewahi kuishi. Kwa kuwa na kitu alichokitaka, Adamu alishindwa. Dhambi zake zilileta mauti na uharibifu, na alifukuzwa Edeni.

Kwa kukosa kwa Adamu ili kuweka haki duniani, Bwana alijipatia hekalu lingine.

"Ndivyo ilivyoandikwa, mtu wa kwanza, Adamu akawa nafsi iliyo hai: Adamu wa mwisho ni Roho yenye kuhuisha. Lakini hautangulii ule wa Roho, bali ule wa asili; baadaye huja ule wa roho. Mtu wa kwanza atoka katika nchi ni wa Udongo. Mtu wa pili atoka mbinguni. Na kama tulivyoichukua sura yake yule wa udongo, kadhalika tutaichukua sura yake yeye aliye wa mbinguni" (1 Wakorintho 15:45-47, 49).

Ujio wa Yesu Kristo ulikuwa ni mwanzo mpya kwa mwanadamu. Hekalu jipya lilikuwa linainuliwa juu kuleta wokovu kwa watu wote; Ingawaje, Huyu Adamu wa pili alikuwa tofauti kabisa na Yule wa kwanza.

"...Yeye hana umbo wala uzuri; na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani. Alidharauliwa na kukataliwa na watu: mtu wa huzuni nyingi, ajuaye sikitiko:Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao, Alidharauliwa wala hakuhesabiwa kuwa kitu" (Isaya 53:2-3).

Kama vile wengi walivyokustaajabia, (sura wake ilikuwa umeharibiwa sana zaidi ya mtu yeyote na umbo lake zaidi ya wanadamu)" (Isaya 52:14).

"Naliwatolea wapigao mgongo wangu, na wang'oao ndevu mashavu yangu; Sikuficha uso wangu usipate fedheha na kutemewa mate" (Isaya 50:6).

Hekalu la mwili wa Yesu Kristo halikuweza kufananishwa na uzuri wa Adamu kabisa ila kama ilivyoahidiwa kwa Israeli, Utukufu wa hekalu lijalo ni mkubwa.

"Yeye akajibu, akawaambia, livunjeni hekalu hili nami katika siku tatu nitalisimamisha. Basi Wayahudi wakasema, Hekalu hili lilijengwa katika muda wa miaka arobaini na sita nawe utalisimamisha kwa siku tatu? Lakini yeye alinena habari za hekalu la mwili wake" (Yohana 2:19-21).

"Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala. Kwa kuwa kama katika Adamu wote wanakufa, kadhalika na katika Kristo wote watahuishwa" (1 Wakorintho 15:20 & 22).

"Maana katika yeye unakaa utimilifu wote wa Mungu, kwa jinsi ya kimwili. Na ninyi mmetimilika katika Yeye aliye kichwa cha enzi yote na mamlaka" (Wakolosai 2:9-10).

Hekalu hili la baadaye lilitwa asili ya mfalme wa Amani. Kwa yeye tunapokelewa kwenye Ufalme na jina liokowao la Yesu li juu ya hekalu lile milele na milele. Kwa hakika utukufu wa hili hekalu lililofuata Yesu unaukuu zaidi ya lile la kwanza.

Hii husababisha mfano wenye kupendeza wa kutimizwa kwa ahadi ya Mungu kwa Zarubabeli. Ingawaje, ahadi ilikuwa pia ni maalumu kwa kutaja "Hii nyumba ya baadaye" katika mahali hapa nitatoa amani." Ahadi ya Hagai 2:7-9 pia

ilitimizwa kikamilifu pamoja na madhara makubwa kwa kanisa na kila mkristo aliyezaliwa mara ya pili.

Ili kuwaza huu utimilifu halisi wa ahadi kwanza lazima tufahamu kuwa ilikuwa siyo lazima iwe inazungumzia jengo maalumu. Hekalu katika wakati wa Kristo na kanisa la Mwanzo lilikuwa ni hekalu la Herode, si lile lililojengwa na Zarubabeli. Njia nyingine anayotoa Hagai 2:9 ni "Utukufu wa mwisho wa nyumba hii utakuwa mkuu kuliko Utukufu wake wa Kwanza". Jambo la muhimu ni kuwa ahadi ilitimizwa katika hekalu la sasa, na Utukufu ulikuwa mkubwa usio na mwisho.

Kutimizwa kwa hadi hii lazima kuwe ilitokea siku ile ya Pentekoste, wakati wanafunzi walipojazwa na roho Mtakatifu. Pia lazima iwe imetokea katika hekalu. Masimulizi yafuatayo ya matukio yanayoongoza kwenye siku ya Pentekoste pamoja na thibitisho chache zihusuzo mji wa Yerusalemu na hekalu itaonyesha jambo hili kuwa ni kweli.

"Natazama, nawaletea juu yenu ahadi ya baba yangu, lakini kaeni humu mjini, hata mvikwe uwezo utokao juu. Akawaongoza mpaka Bethania, akainua mikono yake akawabariki. Ikawa katika kuwabariki, alijitenga nao: akachukuliwa juu mbinguni. Wakamwabudu; kisha wakarudi Yerusalemu wenye furaha kuu. Nao walikuwa daima ndani ya hekalu, Wakimsifu Mungu: Ameni" (Luka 24:49-53).

Mlango wa kwanza wa Matendo unatoa tendo lile la kupaa kwa Yesu na pia inaendelea kueleza juu ya Uteuzi wa Mathia kuchukua nafasi ya Yuda. Katika tukio hili inaelezea kuwa wale kumi na mmoja walidumu katika chumba cha juu na waliendelea na maombi pamoja na wengine, wakati huu Petro alisimama katikati ya wengine, waliofikia kama mia moja na ishirini, na akaleta suala la kumpata mtu mmoja badala ya Yuda (Matendo 1:12-15). Ufahamu wa kimapokeo wa jambo lote hili ni kuwa wote mia moja na ishirini, kuwajumlisha wanawake, wote walikutanika katika chumba cha juu na walikuwa pamoja pale Roho Mtakatifu alipotolewa siku ya Pentekoste. Hata hivyo hii haikubaliani na Luka 24:52, 53 isemayo walidumu hekaluni wakimsifu na kumbariki Mungu. Ilikuwa ni desturi ya Wanafunzi kuabudu hekaluni SIKU YA Pentekoste na baada yake. Matendo mlango wa kwanza hausemi kuwa chumba cha juu; hiyo inasadikiwa tu kwa hakika haiwezekani kabisa kuwa wangetafuta chumba cha ukubwa wa kutosha kuwaweka watu mia moja na ishirini, hasa wanawake walipojumuishwa katika idadi ile na wangehitaji malazi yanayofaa tofauti na ya wanaume. Pia ukitazama wembamba wa barabara za mji wa Yerusalemu ya zamani kwa kweli haiwezekani kuwa Petro angeweza kuhutubia mbele ya watu Elfu tatu mara baada ya Roho kushuka. Tunajua kuwa Petro na Yohana baadaye walihubiri katika ukumbi (Hekalu) la Suleimani na wakapata waongofu elfu tano. Ufinyu wa malazi peke yake kimapokeo linawezekana. Kuwa Roho Mtakatifu alishuka juu na mia moja na ishirini katika chumba cha juu na kuwa Petro alipata waongofu elfu tatu mara baadaye inahitajika nafasi zaidi kidogo. hii inahifadhi kirahisi kama tuna amini Luka 24:53 inaposema kuwa walikuwa hekaluni.

Lengo la jambo lote ni kutimizwa kwa Hagai 2:7-9. Hebu tuchukue mtazamo kuwa wanafunzi walikuwa kwa hakika hekaluni siku ile ya pentekoste na kuona jinsi hili linavyohusiana na ahadi ya Hagai.

"Hata ilipotimia siku ya Pentekoste walikuwako wote mahali pamoja"

(Matendo 2:1).

Huu Umoja kati ya wanafunzi siku ile ya Pentekoste inakumbusha wazi kuweka Wakfu hekaluni la Suleimani, wakati makuhani, pamoja na parapanda mia moja na ishirini, zilikuwa, "kama mmoja wakisikiliza sauti moja ya kumsifu na kumshukuru Bwana" (2 Nyakati 5:13).

"Kukaja ghafla toka mbinguni Uvumi kama uvumi wa Upepo wa nguvu ukienda kasi. Ukajaza nyumba yote waliyokuwa wameketi" (Matendo 2:2).

Itakumbukwa kuwa makuhani walipotoka Patakatifu wingu lilishuka na Utukufu wa Bwana ukaijaza nyumba. Hili lilikuwa katika eneo la hekalu lililojazwa na watu wa kawaida.

Katika ibada ya hekalu wanawake hawakuruhusiwa kuingia ndani na wanaume. Pia hapakuwepo viti katika mahali na pa ndani Ibada. Ingawaje, eneo la nje yeyote angeweza kukusanyika na kulikuwepo viti. Siku ya Pentekoste wanafunzi wangeweza kuwa katika eneo hili la hekalu, na nafasi za ndani zikichukuliwa na wakuu wenye umuhimu zaidi na wegeni.

"Kukawatokea ndimi zilizogawanyikana, kama ndimi za moto uliwakalia kila mmoja wao" (Matendo 2:3).

Katika jinsi ile ile kuwa moto ulishuka katika uwekaji wakfu wa hekalu la Suleimani, Roho Mtakatifu alishuka na ndimi za moto. Kusingekuwa na njia nyingine siku ya Pentekoste itokee nyuma ya sherehe ya hekalu la mwanzo Utukufu wa hekalu lililofuata ulikuwa mkuu kuliko.

"Wote wakajzwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka" (Matendo 2:4)

Hii inatimiza Isaya 28:11-12 na kwa hakika ilikuwa ni kuu kuliko lolote lililowahi kutokea katika hekalu la kwanza. Kwa kweli, ilileta uzuri wa patakatifu pa Patakatifu ndani ya mioyo ya watu kwa mara ya kwanza kabisa, watu walikuwa hekalu la Roho Mtakatifu kwa hakika.

Wayahudi watauwa toka kila taifa chini ya mbingu waliwasikia wakinena, Utukufu wa Mungu katika lugha zao tofauti. Ujumbe wa Petro siku ile ulivuta na kuonyesha toba ya Suleimani, msamaha Mungu aliotoa katika wakfu wa hekalu, na Roho Mtakatifu aliyeijaza nyumba. Amani ambayo Yehova aliahidi kutoa ilihifadhiwa katika kujazwa na Roho Mtakatifu, kwa kuwa kuna "Haki, amani na furaha katika Roho Mtakatifu."

Kwa hakika kitu cha mwanzo kinachoonekana kukosekana siku ile ya Pentekoste ambacho kilikuwepo katika kuweka wakfu wa hekalu la Suleimani ni dhabihu. Ingawaje hili pia lilizidi maelfu ya kondoo na fahali, kwa sababu mwana kondoo wa Mungu amekuja kumwaga damu yake kwa ajili ya dhambi zetu.

Hekalu kule Yerusalemu limebaki ukiwa hivi leo na Wayahudi wamesimama na kuomboleza kuta zake kwa sababu hawakujua siku ya kujiliwa kwao. Ulimwengu mzima waliokombolewa hubeba ndani ya nafsi zao mahali patakatifu pa Ibada, na Roho wa Bwana hukaa ndani ya haya mahekalu yaliyoongezeka, siku ya kuweka wakfu, ila mpaka ahadi iliyotolewa ya kurudi kwa Yesu Kristo. Katika tukio lile kuu haya mahekalu yatabadilishwa na kuchukua Utukufu mkuu kuliko tuliowahi kuujuwa.

MAFUNDISHO YA SHERIA

"Hivyo torati imekuwa kiongozi kutuleta kwa Kristo, ili tuhesabiwe haki kwa imani" (Wagalatia 3:24).

Mpango wa Mungu Unaoendelea usioweza kupinda ulianza na Adamu na ahadi ya mwokozi atakayekuja. Wote waliokuja baadaye walitazamia kutimizwa kwa ile ahadi. Mpaka wakati wa Musa, Mababa walijua tu mawazo ya msingi ya Imani katika Mungu matoleo ya dhabihu kwa ajili ya dhambi zao. Mungu alipompa Musa sheria alipanua ufahamu wao kiasi cha kutosha kuhusu asili yake mwenyewe na kutoa mifano na vivuli vya wokovu utakao kuja.

Mungu wetu wakati wote huhifadhi lililo bora zaidi kuwa la mwisho, wakati wote hutenda kutoka jema kwenda bora na halafu jema kabisa. Kwa sasa tunafurahia uhusiano ambao mwanadamu hajawahi kuwa nao. Kwa mtu kupata kibali mbele ya kiti cha enzi cha Mungu, na Roho wa Mungu hasa akiwa ndani yetu, tuna ushirika wa moja kwa moja na Bwana. Tofauti na mababa, tunajua Jina lake liokoalo na kushiriki maelezo ya ufahamu ule ule ambao manabii wangetoa mkono wao wa kuume ili kuwa nayo. Yote kutambulikana kwa usiku mmoja ila yalitokea zaidi ya mamia ya miaka ya usimamizi wa maandalizi. Kidogo kidogo sheria na manabii vilituongoza kwa Yesu.

"Kwa maana ni amri juu ya amri, amri juu ya amri: Kanuni juu ya kanuni, huku kidogo na huku kidogo" (Isaya 28:10).

Ufahamu mzuri wa kazi ya msingi iliyowekwa na sheria itatupa msingi imara kwa kufahamu mpango wa Mungu wa wokovu leo.

Kujifunza kikamilifu mpango wa Hema ya jangwani linaloweza kurefushwa na kuhusisha nukuu. Kila rangi ya ya vifaa vya Ujenzi, vipimo na kadhalika,i ina Ishara yake maalum. Ingawaje, Ujuzi wa Kimsingi kabisa wa Hema lilikuwa ni nini na kitu gani kilitokea pale yapo mengi ambayo ni muhimu ya kujipatia ufahamu wa kutosha.

Hema kule Jangwani lilikuwa kimsingi ni hema tu ambalo lilihudumu kama hekalu lenye kuhamishika, Utaratibu kamili wa makuhani, Walawi, n.k. Ulipangwa kushughulikia Usimamishaji, Upanguaji na kusafirisha Hema vile vile kufanya kazi takatifu kama vile kutoa dhabihu na kusimamia sheria. Hema kihalisi ilikuwa ni kituo cha shughuli kwa Waisraeli. Makabila tofauti walipiga kambi kulizunguka Hema. Kulikiwa na matoleo kwa ajili ya dhambi, Utakaso, matoleo ya amani na pia mambo yote ya muhimu ya siku ya Upatanisho Hema lilikuwa muhimu kwa wokovu. Ilikuwa ni ndani ya hema tu dhambi ziliweza kufunikwa.

Jinsi watu wa Israeli walivyokaribia hema walikutana kwanza na madhabahu ya dhabihu iliyotengenezwa kwa shaba na kubwa kiasi cha kuchukua ng'ombe mzima. Ilizuia kuendelea zaidi ndani ya hema, Mnyama aliuwawa na damu kukusanywa ili kutumika kwa ajili ya Utakaso. Waebrania 9:22-28 hutueleza kuwa, kama vile Hema lilivyotakaswa kwa damu ya dhabihu, tunatakaswa kwa damu ya Yesu. Madhabahu ya shaba halikuwa eneo la kupendeza. Maumivu makali ya ng'ombe au kondoo dume anayekufa iliisambaza madhabahu damu kama vile vile haikuruhusiwa kuingia ndani ya hema pasipo mauti ya dhabihu ndivyo kusivyoruhusiwa kuingia katika Ufalme wa Mungu pasipo kufa mauti ya toba.

"Tuseme nini basi? Tudumu katika dhambi ili neema izidi kuwa nyingi? Hasha! Sisi tulioifia dhambi tutaishije tena katika dhambi?" (Warumi 6:1-2).

Baada ya kukamilisha kikamilifu dhabihu, kuhani aliiendea Birika la maji.

Hili liliwekwa katika kuingia mahali patakatifu. hapa kuhani aliosha damu inayochuruzika toka mikononi mwake, akijitakasa katika maandalizi ya kuingia Patakatifu. Hili ilitengenezwa kwa shaba iliyosuguliwa ili kuhani aweze kuona katika muonekano wake madoa yote yaliyohitaji kuondolewa. Hii moja kwa moja huonyesha ubatizo.

"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya Utukufu wa baba, Vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima" (Warumi 6:4).

Kuingia Patakatifu kuhani alivuka taa ya dhahabu, wakati mwingine iliitwa kinara cha taa cha dhahabu. Hiki kilikuwa ni kipande cha chombo kilichotengenezwa kwa dhahabu safi. iikuwa ni mfano wa nuru ya Roho wa Mungu, ambayo hasa ni sababu ya sehemu ya wokovu wetu. Dhahabu inafananishwa na usafi. Mafuta yaliyotumika katika taa ni mfano mwingine wa Roho Mtakatifu.

Pembeni mwa kinara cha taa ya dhahabu kulikuwako meza ya mikate ya wonyesho. Meza hii tena ilkuwa ya dhahabu halisi. Juu yake uliwekwa mkate kwa ajili ya ukuhani. Huu kwa vyovyote unawakilisha Neno la Mungu na pia huduma. Kwa kupokea nguvu na nuru kwa mwelekeo, kuhani aliweza kuendelea.

Upande mwingine wa pepembezoni pa mahali patakatifu ilisimama madhabahu ya uvumba. Hiki chombo cha dhahabu kinawakilisha kazi ya maombi na ibada katika wokovu wetu. Kuhani alileta moto toka madhabahu ya shaba kuchomwa uvumba. Uvumba wenyewe ulitengenezwa maalumu kwa mchanganyiko wa vitu vilivyotumika kwa kusudi hili.Uvumba ulitakiwa kupondwapondwa na kuwa unga ili uwake vizuri na kutoa harufu ya kupendeza iliyopokelewa kwa Mungu. Hii ishara ya maombi ilimfanya mtu asahau uvundo na damu ya madhabahu ya shaba, haikuwezekana kabisa pasipo moto toka madhabahuni.

Nyuma tu ya madhabahu ya Uvumba kulikuwa na pazia la kupendeza lililomtenga kuhani na Patakatifu pa Patakatifu. Hili pazia lilikuwa na Imara sana. Lilikuwa ni mfano wa mwili wa Kristo. Kama vile mwili wa Kristo ulivyoweka ukamilifu wote wa uungu, Pazia lilikuwa ni ukuta wa nje wa Patakatifu pa Patakatifu, ambapo uwepo wa Mungu ulitokea kwa nyakati maalumu. Pazia lilipasuka kutoka juu mpaka chini katika siku ile ya kusulubiwa, ikionyesha kuwa Mungu mwenyewe amefungua njia kwa wanadamu wote kuingia katika uwepo wake.

Nyuma ya pazia kulikuwa na mahali panapoitwa Patakatifu pa Patakatifu. Chombo pekee kilicho hapa kilikuwa na Sanduku la Agano. Hili lilikuwa ni kasha la mbao iliyofunikwa kwa dhahabu. Ilihifadhi jiwe la mbao za sheria, chungu cha mana na fimbo ya Haruni ile iliyochipuka. Juu ya kasha hili walikuwapo malaika wawili wa dhahabu waliokitia kivuli kiti cha Rehema ilikuwa ni hapo ambapo kuhani mkuu alimimina damu ya dhabihu siku ile ya upatanisho. akifanya upatanisho, kwa dhambi za Israeli. Hii ni namna ya Upatanisho uliofanywa na Yesu Kristo kwa ajili Yetu.

"Kwa sababu Kristo hakuingia katika patakatifu palipofanyika kwa mikono, ndio mfano wa Patakatifu halisi: bali aliingia mbinguni hasa, aonekane sasa usoni pa Mungu kwa ajili yetu. Kadhalika Kristo naye akiisha kutolewa sadaka mara moja

azichukue dhambi za watu wengi, atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao

wamtazamiao kwa wokovu" (Waebrania 9:24, 28).

SIKUKUU ZA WAYAHUDI

Mlango wa ishirini na tatu wa mambo ya Walawi inatueleza sikukuu tofauti ambazo zilikuwa ni za muhimu, matukio ya kidini kwa Israeli. Zilikuwa zinahusu ukumbusho wa mambo makuu Mungu aliyofanya kwa Israeli, Pia kutoa njia ya msamaha wa dhambi zao na kufunikwa. Baadhi zilikuwa ni nyakati za kufurahia, nyingine zilikuwa ni nyakati za mateso na kuchunguza moyo. Zote zilikuwa za muhimu kwa mambo ya kiroho ya Wayahudi. Vivyo, kama Wagalatia 3:24 inatueleza, zinatusaidia kutuongoza kumfahamu Kristo.

PASAKA

Waisraeli walipokombolewa toka Misri Mungu aliwapa Ulinzi wa ki Mungu kutokana na malaika wa kifo. Kwa kifo ya mwana kondoo wa pasaka aliyekuwa badala ya mzaliwa wa kwanza wa kila nyumba, aliepushwa kutokana na kifo iliyoishukia Misri yote. Njia ya ukombozi huu ulikuwa ni utii kwa mpango ambao Mungu aliutoa kwa Musa. Utii kwa Mungu bado ni njia pekee ya wokovu.

Kitabu cha kutoka Mlango wa kumi na mbili unatupa maelezo ua undani ya Pasaka. Mwana kondoo alichinjwa kwa kila nyumba au labda aliliwa na nyumba ndogo mbili.

Baadaye damu iliwekwa katika miimo ya kizingiti cha mlango. Usiku ule walitakiwa kuwa ndani tu, kumchoma mwana kondoo na kumla. Hakikutakiwa kusazwa chochote, ilitakiwa aliwe wote kabisa. Waliambiwa wale huku wamevaa viatu vyao na mizigo yao ikiwa mikononi mwao.

"Na ile damu itakuwa ishara kwenu katika zile nyumba mtakazo kuwemo; nami nitakapoiona ile damu, nitapita juu yenu, lisiwapate pigo lolote litakalo waharibu, nitakapoipiga nchi ya Misri" (Kutoka 12:13).

Ukombozi huu kutoka Misri ni mojawapo ya mifano bora ya wokovu. Misri ni ulimwengu katika mfano huu, na Kristo ni mwana kondoo. Wokovu wetu unaweza kutokea tu tunapotii maelezo ya sasa ya Bwana kwa kutumia damu yake katika hali yetu. Mauti inazungumza kuhusu toba. Pia imetajwa kuwa huu ungekuwa ni mwanzo mpya, siku mpya kwa Israeli. Toba ni hatua ya kwanza ya muhimu katika safari ndefu toka hukumuni kuelekea ukombozi. Kama Wayahudi walivyotakiwa kukumbuka huu mwanzo kwa sherehe ya ukumbusho kila ,mwaka toba wakati wote ipo pamoja nasi. Mpaka tufikie ukamilifu hatuwezi kuacha kutubu na kutegemea damu ya mwana kondoo.

Haishangazi wakati Yesu alipokuja kwa Yohana Mbatizaji alipokelewa na, "Tazama mwana kondoo wa Mungu, aichukuaye dhambi ya Ulimwengu!" Yesu alisulubiwa katika siku ya sikukuu ya Pasaka, alitolewa mara moja na kwa milele.

MIKATE ISIYOCHACHWA

Mambo ya Walawi 23:6-8 inaweka sikukuu ya mikate isiyotiwa chachu. Siku inayofuata sherehe ya Pasaka, Waisraeli, wote walitakiwa kula mikate isiyotiwa chachu. Hii ilidumu kwa siku saba, siku ya kwanza na siku saba zilikuwa siku

takatifu au sabato, ambazo walitakiwa wasifanye kazi. Hii inaeleza kwa hakika kuwa Wayahudi walitaka Yesu aondolewe toka kwenye msalaba, kabla ya kuzama kwa jua kwa kuwa siku ya baada ya pasaka ilikuwa ni Sabato. Mikate isiyochachwa ni isiyo na hamira, mfano wa uhai. Mikate isiyochachwa ni mfano wa mauti ya Yesu. Pia, inaonyesha mauti ya nguvu ya dhambi ndani ya maisha yetu. Katika sikukuu ya mikate isiyochachwa, Yesu alikuwa kaburini, amezikwa. Kufuatia mauti ya toba pia sisi tunazikwa pamoja naye katika ubatizo (Warumi 6:3-4).

MALIMBUKO

Katika mambo ya Walawi 23:9-11 Mungu aliwapa Israeli Sikukuu ya malimbuko. Sherehe hii ilikuwa ni kusherekea uhai walileta machipukizi ya kijani ya kwanza, Majani ya ngano n.k. na Kupunga mbele za Bwana. Ni kwa kawaida tu kuwa baada ya ukombozi kutoka mauti ndipo kusherekea uhai kunafuata. Hii ilitokea siku inayofuatia sikukuu ya mikate isiyochachwa, ambayo ndiyo siku Yesu alifufuka toka kwa wafu.

"Lakini sasa Kristo amefufuka katika wafu, limbuko lao waliolala" (1 Wakorintho 15:20).

"Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya Ubatizo katika mauti yake, kusudi kama kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa baba vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake" (Warumi 6:4-5).

Kufufuka kwetu toka mautini huja pamoja na utoaji wa uhai unaotolewa kwa kujazwa Roho Mtakatifu. Yesu anasema kuwa alikuja ili tuwe na uzima, na kisha tuwe nao tele. Hii inaletwa kwa Roho Mtakatifu. Tumaini letu la ufufuo wakati wa Unyakuo wa kanisa ni kuwa Roho Mtakatifu anakaa ndani yetu.

"Lakini ikiwa Roho wake yeye aliyemfufufa Yesu katika wafu anakaa ndani yenu, yeye aliyemfufua Kristo Yesu katika wafu, ataihuisha na miili yenu iliyo katika hali ya kufa, kwa Roho wake anayekaa ndani yenu" (Warumi 8:11).

PENTEKOSTE

Kwa njia nyingine inaitwa sikukuu ya majuma, hii sikukuu ni kusherekea Mavuno. Siku ya hamsini baada ya sikukuu ya malimbuko (Mambo ya Walawi 23:15-17), Waisraeli walileta mikate iliyochachwa kupunga mbele za Bwana. Hii kazi iliyomalizika ya mavuno ilisherekewa kama mfano wa kazi ya wokovu iliyofanywa na kristo na kanisa lake.

Siku ya Pentekoste, wakati Wayahudi walikuwa wanasherehekea sikukuu ya Pentekoste, Roho Mtakatifu alishuka juu ya Wanafunzi, Ikiashiria mwanzo wa mavuno. Kilio cha Yesu katika huduma yake ilikuwa ni watenda kazi kwa ajili ya mavuno. Kuweka chachu ndani ya kanisa kwa nguvu ya Roho Mtakatifu.

"Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu Roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Matendo 1:8).

Haistaajabishi mwisho hautakuja mpaka Injili hii imehubiriwa kama

ushuhuda kwa kila taifa. Hii ni kazi ya mavuno na utimizo wa sikukuu ya Pentekoste.

BARAGUMU (Tarumbeta)

Bwana aliendeleza elimu yake ya Israeli kwa kuwapa sikukuu ya Matarumbeta (Mambo ya Walawi 23:23-25). Kwa kwaida tarumbeta zilipigwa Israeli kwa sababu tatu; kuashiria mwisho wa mavuno, kuwaita Wafalme pamoja na kuonya kwa siku ya Upatanisho inayokaribia.

"Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao walikufa katika Kristo watafufuliwa kwanza kisha sisi tulio hai, tuliosalia tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani na hivyo tutakuwa na Bwana milele" (1 Wathesalonike 4:16-17).

SIKU YA UPATANISHO

Kwa kipindi cha siku kumi Israeli ilikuwa atese nafsi yake katika mandalizi kwa Siku ya Upatanisho (Mambo ya Walawi 23:26-32). Siku ya upatanisho kuhani mkuu alichukua damu ya dhabihu kamili na isiyo na kosa na kuipeleka Patakatifu Pa Patakatifu kufanya Upatanisho kwa dhambi za Israeli. Kama walimtii Bwana katika kuungama dhambi zao na kuleta uwepo wa Bwana ujaza Patakatifu pa Patakatifu na Israeli walitambua msamaha wao. kama vile kuhani alipoingia Patakatifu pa Patakatifu, ndivyo hivyo watakatifu wanavyoingia Patakatifu halisi, na wokovu wao utakuwa hakika.

MAHEMA

Mambo ya Walawi 23:33-43 inatuambia kuhusu wakati wa kufurahia na kusherekewa kwa amani. Watu wa Israeli walifanya vibanda kutoka matawi ya miti wakaishi ndani yake. Kwa siku nane watu walifurahia na kukumbukwa kuwa walikuwa katika utumwa Misri. Hii sikukuu ilifuatia mwisho wa mavuno na ulikuwa ni wakati wa kupumzika na kufurahia. Ni tumaini la namna gani lililo mbele kwa ajili ya watoto wa Mungu! Mavuno yatakapokwisha. Atafuta machozi kutoka machoni mwetu, hakutakuwepo na mauvimivu, huzuni ni kufurahi tu milele katika nyumba ya Baba yetu. Pale tutatazamana kufurahi kwa ukombozi wetu toka kifungoni. Wokovu huu wetu sisi siyo jambo la kushangaza sana. Ni dhahiri na kuthibitishwa tena na tena ili kwamba pasikuwepo na shaka.

Mambo mengi sana ya sheria yanatuonyesha rehema na wema wa Bwana, miji ya makimbilio, mwaka wa Yubilee, Mwaka wa kuwekwa huru na sehemu nyingi zaidi za sheria zinatuonyesha wokovu wetu zaidi za sheria linabaki ili litajwe kwa sababu ni elezo dhahiri la ushirika kati ya Kristo na Kanisa: Mkombozi wa Jamaa.

MKOMBOZI WA JAMAA

Biblia inatoa kielelezo kwa ajili yetu pendo kuu na msaada ambao Kristo hutoa kwa Kanisa Lake katika wazo la Mkombozi wa Jamaa.

Kwanza kabisa hakuna shaka kuwa amechukua nafasi ya mkombozi wetu wa jamaa. Je yeye siye mzaliwa wa kwanza kati ya ndugu wengi, Rafiki aambatanaye na mtu kuliko ndugu?

Wajibu mkuu wa Mkombozi wa jamaa ulikuwa kununua jamaa yake toka kwenye utumwa na kulipizia kisasi damu yake. Kama mtu alikuwa maskini na akajiona inambidi awe mtumwa ili aishi, basi mkombozi wa jamaa alitakiwa kununuwa uhuru wake (Mambo ya Walawi 25:25). Kama mtu alikufa na kuacha nyuma yake mali na mke, mkombozi wa jamaa alitakiwa kutunza ule urithi ili usitoweke na kama inawezekana kumwoa mwanamke kumwinulia watoto marehemu (Ruthi 4:1-4). Ni mfano gani unaofaa kuliko kumwona Kristo kama mkombozi wetu. Alilipa gharama kwa ajili ya uhuru wetu tulipokuwa tumeuzwa chini ya dhambi. Alitutwaa kuwa Bibi Harusi wake tulipokuwa fukara na kupotea.

Kama mtu aliuwawa ilikuwa ni wajibu wa mkombozi wa jamaa kutwaa kisasi kwa kifo chake (Hesabu 35:12). Baada ya kuonekana na hatia muuaji alitolewa na kuwekwa mkononi mwa mkombozi wa jamaa ili auwawe, ili kulipa kisasi cha kifo cha jamaa yake. Mungu akasema "Kisasi ni changu, nitajilipizia". Siku moja Yesu atamkamata shetani na kumtupa katika ziwa la moto. Adui yetu ataangamizwa kwa nguvu ya mkombozi wa jamaa yetu.

Inasemekana kuwa wakati mwi-Israeli alikuwa anafukuzwa na adui yake angeliita jina la mkombozi wake wa jamaa, mlipa kisasi wa damu. Kwa mamna hii kama aliuawa ilikuwa ni kazi ya mtwaa kisasi kumtafuta muuaji na kulipa kisasi kwa kuua, kwa hiyo kama mtwaa kisasi wake alikuwa mtu mwenye nguvu, adui angeweza kufikiria mara mbili kuhusu alichokuwa anakifanya aliposikia lile Jina. Haishangazi maandiko yanaposema kuwa jina la Bwana ni ngome imara, wenye haki hukimbilia wakawa salama! Adui yetu anajua na kuliogopa Jina la Yesu. Mara nyingi tunaokolewa toka ghadhabu ya shetani kwa nguvu ya Jina hilo.

"Wala hakuna wokovu katika mwingine awaye yote, kwa maana hapana jina jingine chini ya mbingu walililopewa wanadamu litupasalo sisi kuokolewa kwalo" (Matendo 4:12).